# *Mjumbe Wa Jioni*

Asanteni, sana. Bwana awabariki.

Mwaweza kuketi.

2 Mwanangu alinijia leo hii, akasema, “Baba, laiti tungalikuwa tumeliona kanisa hilo kabla hatujaanza kujenga letu, ni mahali pa kupendeza sana.” Naye akazungumza kuhusu...Kasema, “Sijakutana na huyo mhudumu bado, bali kama yeye ni mtu mwema kama mke wake, hakika ni mtu mzuri.” Kwa hiyo tuna furaha kuwa hapa.

3 Nami ni—ninautarajia u—ule mkutano usiku wa leo, ambapo Mungu atamwaga baraka Zake juu yetu na kutusaidia.

4 Sasa sisi ni...Ndio kwanza niingie, nami nikamsikia Ndugu Williams, ninaamini, akisema jambo fulani kuhusu kuwa Ramada. Pia nadhani matangazo yamefanywa, kuhusu hilo. Kwa kawaida wao hushughulikia hayo kabla sijaingia. Na bila shaka tunautazamia wakati mkuu huko chini mkutanoni. Nayo sehemu yangu hapa ni kwa namna fulani kuzunguka tu na kukutana na ndugu na kufanya ushirika miongoni mwa watu, na kuomba ya kwamba Mungu atatupatia na—namna nzuri ya mwamko, halafu basi tunaweza kwenda moja kwa moja katika Ramada katika mkutano mkubwa. Na kwa hiyo tunajaribu kuyatembelea makanisa yote tuwezayo, mpaka wakati huo. Nasi tuna wakati mzuri sana. Hakika tuna wakati wa ajabu pamoja na ushirika miongoni mwa ndugu zetu.

5 Na kwa kawaida mimi...Mtu yeyote anajua mimi si mhubiri mzuri, mimi kidogo ni tairi tu ya akiba. Lakini mimi—mimi...Huduma yangu ni kuwaombea wagonjwa. Nami... Tumekuwa tukisongamana sana usiku, na kadhalika, hata ni vigumu kwetu kupata nafasi ya kutosha kufanya hivyo. Nasi tutajaribu kama tutaninii...tutakapofika mahali tunapoweza, humu ndani, kusambaza kadi na kuwaleta hao watu ndani na kuwaombea. Lakini tukiwa na mkutano mmoja usiku kwa wakati mmoja, wale usingeweza kuwafikia usiku wa leo basi wangewasukumia moja kwa moja mahali fulani kesho yake usiku, na huko nyuma sana mahali pengine, kwa hiyo kwa njia hiyo kidogo nimefanya mazungumzo ma—mafupi—mafupi kila usiku kwa ajili ya watu, na vizuri niwezavyo kidogo kwa... kwa ajili ya heshima na utukufu wa Yesu Kristo, na kwake Yeye ambaye sote tunampenda na kumwamini, na ushirika wetu pamoja.

6 Nadhani mlisikia habari za ile ajali pale pembeni, muda mfupi tu uliopita. Sijui kama mtu huyo aliuawa, ama kwamba alikuwa ni nani, hilo gari lilipita. Tulisimama tu, maombi mafupi tu, dakika chache zilizopita. Yapata majengo mawili

juu hapa kulikuwako na mtu fulani aliyekuwa amegongwa kando na kusukumwa kote mtaani. Na mtu mkubwa alikuwa amefunikwa huko nje. Nao askari walikuwa pale, bali sidhani gari la kuchukulia wagonjwa lilikuwa limefika pale bado. Wao hapana shaka . . . Kama hakuuawa, hakika ilikuwa . . . Aligongwa upande *huu* na kupondwa kote kupitia mlangoni upande huo mwingine, kwa hiyo hapana shaka lilikuwa ni pigo kubwa mno. Mwajua, linaninii tu . . .

7 Lazima tumtumikie Mungu kila dakika. Hatujui ni wakati gani—hatujui ni wakati gani ambapo mambo hayo yangeweza kutukia. Labda tunafikiri haitakuwa ni sisi, lakini mnajua inaweza ikawa, mwajua. Kwa hiyo, ninaamini Yesu alisema, "Iweni tayari," kwa kuwa hatujui ni dakika ipi ama saa ambayo tunaweza kuitwa. Ndipo tutaenda mahali ambapo hawana ajali, wala masumbuko. Tunashukuru sana kwamba kuna mahali kama hapo katika ahadi.

8 Mwajua, wazo lenyewe, usiku wa leo, la—la kuona ya kwamba tungekuwa na shauku ya mahali kama hapo, hiyo inaonyesha kuna mahali kama hapo. Mnaona? Nasi tunajua kwamba negativu zote, vivuli vyote, inabidi pawe na kitu fulani cha kusababisha kivuli. Kivuli ni uakisi. Kwa hiyo kukiwa na uhai kama huu, inathibitisha ya kwamba ni kivuli, basi kuna uhai halisi mahali fulani ambapo huu ni uakisi wake. Mnaona? Unaona mti, jinsi mti ulivyo wa kupendeza. Basi mnajua huo ni nini? Ni negativu ya mfano wake, kivuli, cha ule Mti wa Uzima Mbinguni.

9 Sasa, mnajua, wakati Mungu alipokuja duniani, wakati alipokuwa akiatamia juu ya nchi hapo mwanzo, na labda kitu cha kwanza kilichotokea kilikuwa ni ki—kiluwiluwi, kama vile wanasayansi wanavyojaribu kusema. Cha pili huenda kilikuwa ni kitu fulani . . . Naamini katika mageuzi ya kweli ya Kikristo, bali siamini wote ulitokana na seli moja. Ninaamini ilininii tu . . . Mungu aliumba kiluwiluwi, na kisha akaumba samaki, na halafu akaumba kitu kingine. Na ninii tu . . . Ninaamini katika kutokea, sio kwa seli ile ile, bali kiumbe tofauti wakati wote.

10 Na hatimaye akaendelea, kutokea kwa spishi ya juu zaidi, basi baada ya kitambo kidogo ikamwakisi Yeye aliyekuwa akiatamia, ambaye alikuwa ni Mungu. Sasa, kuthibitisha hiyo ni kweli, wakati Mungu alipofanyika mwili ilikuwa ni Yesu Kristo, mwanadamu. Mnaona? Kwa hiyo, sio Malaika, mwanadamu. Kwa hiyo inaonyesha ya kwamba ilimwakisi Yeye.

11 Na, loo, Biblia hii ya kale imejaa hivyo vito vya kale vya thamani. Ninaninii tu . . . Ninapenda kutafuta madini (nanyi je?) na kuingia tu mle na kutikisa na kupangusa mavumbi yote kutoka Kwake, na kuiangalia nione ni kitu gani Hicho. Jinsi ambavyo vito, ninyi watu mnajua jinsi ambavyo hapa Arizona, vito vikuu hutoka katika mavumbi ya nchi. Huko ndiko

vinakotoka. Na vito vya Mungu hutolewa katika mavumbi, pia. Na Yeye. . . Tuna furaha sana kwamba Yeye hutupa majaliwa ya kuingia kwenye kiwanda Chake kikuu cha kusafishia, na takataka zote zinaondolewa.

12 Mnajua jinsi walivyokuwa wakifanya? Hakika, ninyi watu wa Arizona mnajua jinsi hao. . . kabla hawajawa na mashine ya kuyeyushia madini, jinsi ambavyo walikuwa wakisafisha dhahabu. Tunaambiwa kwamba walichukua dhahabu na kuipiga. Wahindi wa kale walikuwa wakifanya hivyo, kuipiga. Na kuipindua tu, na kuipiga na kuipiga, mpaka wakapiga na kutoa takataka yote kwake. Na jinsi walivyojua kwamba yote ilikuwa imekwisha (kimbwi yote na kadhalika iliyo ndani yake, yote hiyo), wakati walipojua vipi, huyo mpigaji aliuona uakisi wake ndani yake, angeweza kujiona mwenyewe. Ndipo akajua ilikuwa ikitakasika, wakati ilipoiakisi sura yake mwenyewe.

13 Basi, mwajua, nafikiri Mungu anataka kulifanya Kanisa Lake hivyo, aupige tu ulimwengu wote utoke mpaka uakisi wa Yesu Kristo unaishi katika kila mmoja wetu nasi tunauakisi Uzima Wake. Ndipo tuko tayari basi kwa ajili ya ninii Yake. . . Yeye anajiakisi Mwenyewe kupitia sisi wakati huo, tunapopata. . . tunapoweka kando kila mzigo na dhambi ituzingayo kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa subira mashindano yaliyo mbele yetu, tukimwangalia yule Mfano, Mwanzilishi na Mwenye Kuitimiza Imani yetu, Yesu Kristo. Nina furaha sana kwa Hiyo!

14 Sasa, kwa kawaida mimi husema kila usiku. . . Nilimwambia Ndugu Carl Williams, nikasema, "Ndugu Carl, hao watu hawataki kunisikiliza tena, huku na huku kupitia hayo mabonde, nikiwaweka mpaka saa mbili au tatu wakati wa usiku."

Akasema, "Vema, vema, njoo."

15 Kwa hiyo ninaithamini subira yenu katika—katika kunialika nirudi tena. Na sasa kila usiku. . .

16 Nilizungumza na mke wangu muda mfupi uliopita, huko chini. . . Yuko Tucson sasa, na mimi nikasema, "Hali ya hewa ikoje?"

17 Akasema, "Inapata joto." Kisha akasema, "Hivi unaweka ratiba?"

Nikasema, "Kikamilifu kabisa, yapata saa nne ama tano kila usiku."

18 Nikamwambia, "Nitapumzika kiasi wakati nitakapoenda huko Arizona wakati huu kwenye mkutano huu mdogo. Ninaenda kwenye makanisa hayo, hao ndugu. Sitawaadhibu watu hao, nitaenda mle tu na nitaacha uimbaji ufanywe, ile yubile. Nitajikatiza, nipunguze muhtasari wangu kufikia kama

dakika kumi na tano, ishirini, tuseme 'Amina' na kwenda nyumbani."

Akasema, "Unaweka ratiba?"

19 Nikasema, "Naam, mpenzi, ninaiweka; ratiba ya kawaida, kufikia saa tatu." Watu wazuri sana; subira tele.

20 Vema, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa tunapomkaribia Yeye. Sasa, nina hakika kwamba katika kusanyiko zuri la watu kama hawa wanaoamini, na hasa sana...Ninaona vitanda viwili vya wagonjwa vimewekwa hapa, watu walio wagonjwa na wahitaji, ninajua wana haja maalum. Hapana shaka ila kuna wengine wengi walio na haja hizi. Kama ndivyo, inueni tu mikono yenu na hebu ijulikane tu unapoinua mkono wako. Na sasa katika maombi nitaenda kule na kuwaombea watu hawa katika vitanda hivi vya wagonjwa wakati—wakati tukiwa hapa, kusudi tuwe na hakika ya kulipata. Kama jambo fulani likitukia...Walikuwa waaminifu vya kutosha kuletwa hapa ndani, ninawatakeni ninyi nyote mwombe pamoja nami.

21 Baba yetu wa Mbinguni, tunaweka kando sasa kila wazo lingine, tukizitakasa nia zetu, nasi tunakuja katika Uwepo Wako kwa ajili ya kusafishwa kwa nafsi yetu. Nasi tunaleta mbele zetu Damu ya Bwana Yesu. Tunakiri kwamba hatustahili baraka yoyote ambayo Wewe ungetupatia, lakini kwa kuwa Yeye alikufa kusudi tupate baraka hizi, na umetwambia tuje kwa ujasiri mbele ya Kiti cha Enzi, kwamba tuna njia ya kuzifikia baraka hizi kupitia kwa neema ya Bwana wetu Yesu, Yule aliyekuja duniani, Imanueli, na kupachukua mahali pa mwenye dhambi. Yeye alifanyika *sisi*, loo, tupate kuwa *Yeye*.

22 Ni badilisho la jinsi gani, Bwana! Maisha ya dhambi, yaliyoelekea kuzimuni tuliyokuwa nayo, na kujua kwamba Mmoja alikuja na kujitwika maisha hayo juu ya nafsi Yake, na kuzitakasa dhambi zetu kwa Damu iliyomwagika ya Uhai Wake Mwenyewe. Ni zaidi ya vile mioyo yetu ingaliweza hata kuliwazia, Bwana. Halafu basi, mbali na hayo yote, Yeye alifanya njia ya kuondolea mbali uovu wetu na kutuponya kwa kupigwa Kwake. Tunashukuru sana ya kwamba Yeye aliahidi ya kwamba angetuweka vema wakati tukimtumikia.

23 Na sasa usiku wa leo, Baba, kuna haja nyingi ambazo zimeninii...huku mikono yao imeinuliwa. Tunajua ya kwamba Wewe utazingatia kila moja ya hizo, ukijua ni nini kilicho chini ya huo mkono, moyoni.

24 Pia ninaomba, Bwana, kwamba Wewe utalikumbuka Neno usiku wa leo tunapolisoma; na kutafakari juu Yake kama somo dogo, kama shule ya Jumapili, ili tuweze kuondoka hapa usiku wa leo na—na kuwa na hili mioyoni mwetu, kwamba tunajisikia kwamba tungekuwa karibu zaidi na Wewe, tukitoka, kuliko tulivyokuwa hapo tulipoingia. Hiyo ndiyo sababu sisi

tupo hapa, ili iweze kuleta uamsho kote nchini, pasipo kujua ni lini hasa utakapoanza, ila kwa matarajio tunautazamia, Bwana. Tunaweka mbele kila jitihada ya kibinadamu tujuayo jinsi ya kuleta uamsho unaomleta mwanamume na wanawake, wavulana kwa wasichana, kwenye maarifa ya kuokoa ya Kristo.

25 Tunataka kukushukuru kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya mchungaji wake mwema na familia yake, na kwa ajili ya mashemasi wote, wadhamini, na kwa yote linayowakilisha. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya wale wenye ujasiri wa kulitetea. Pia, Bwana, tunaomba tu baraka za Mungu zikae juu yao. Bariki kila jitihada. Jalia hiki kiwe ni kituo, Bwana, ambapo bonde lote hapa linaweza kuingia na kupata raha. Tujalie, Baba. Jalia maombi ya mchungaji yajibiwe kwa ajili ya wagonjwa. Jalia maombi yake yajibiwe kwa ajili ya wokovu, kwa ajili ya wote wanaoingia ndani—katika maeneo ya Injili. Baraka Zako na ziwe juu yake. Pia jalia kanisa lisipungukiwe na karama yoyote ya kiroho, jalia pawe ni mahali, kanisa mfano kwa jamii nzima. Tujalie, Bwana.

26 Sasa, Baba, huku wamelala kwenye vitanda vya wagonjwa hapa usiku wa leo, wasioweza kuketi na kuufurahia mkutano, ni wale wasio na majaliwa haya. Nao wameletwa hapa kwa njia fulani, usiku wa leo. Ee Mungu, uwarehemu! Nawazia, "Vipi kama huyo alikuwa ni mke wangu ama ndugu yangu, ama mtu fulani wa jamaa, ambaye nilimfahamu vizuri sana?" Ni wa mtu fulani, nami ninaomba, Baba, kwamba neema ya Mungu, pamoja na nguvu Zake, zitashuka katika ukombozi wa Kiungu kwa ajili yao usiku wa leo, na kuwakomboa kutoka kwenye vitanda hivi vya wagonjwa. Jalia wasiwe kwenye vitanda hivi vya wagonjwa muda mrefu zaidi ya mkutano huu usiku wa leo. Jalia, watakapoondoka, vitanda vya wagonjwa viachwe nyuma. Jalia zile nguvu, zilizomfufua Yesu katika wafu, zihuishe miili yao kwenye afya mpya na nguvu tena. Tujalie, Baba yetu. Sasa, tunajua ya kwamba Wewe uliahidi kufanya hivyo.

27 Kwa hiyo, imeandikwa katika Maandiko, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

28 Sasa, Baba, kwamba kusiwe na mtu yeyote wanayeweza kumfikia, wakati wengine wanaweza kufikiana, nitashuka chini katika kumbukumbu la amri hii. Pia, Mungu, nitatarajia kupokea barua kutoka kwao, kwamba lilitukia, kwa kuwa ninaenda katika Jina la Yesu Kristo.

29 [Ndugu Branham anaondoka jukwaani kwa dakika tatu na nusu kuwaombea wale walio kwenye vitanda vya wagonjwa, maneno yake hayasikiki—Mh.]

Bwana, naamini, Ee Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana, Bwana, naamini;

Bwana, naamini, Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana, Bwana, naamini.

30 Kwa kuwa hao mama wote wawili walikuwa na vivimbe, kansa kwa mmoja, basi, afadhali upesi nitoe ushuhuda huu mdogo, kama itanibidi kukatiza baadhi ya mazungumzo yangu. Kabla tu ya kuondoka nyumbani, kisa cha mwisho nilichokuwa nacho kabla ya kuondoka, hicho kilikuwa ni kisa cha ajabu sana, kulikuwako na mama fulani na jina lake ni Dyer; alikuwa, ninasahau jina lake sasa. Ilikuwa ni Daktari Dyer, kutoka Louisville. James fulani, Daktari James Dyer, mtaalamu wa vivimbe, na kadhalika, huko Louisville.

31 Binti yake alicheza piano katika kanisa la Mlango Wazi, ambamo Daktari Cauble ndiye mchungaji; ninii tu, loo, sinagogi kubwa mno la kale la Kiyahudi. Naye mtu huyo mwenyewe alikuwa ni mfuasi wa Church of Christ, Church of Christ la kimadhehebu, naye aliongoka akaiamini injili ya full Gospel, mtu mzuri sana. Basi yeye alicheza katika mkutano wangu nilipokuwa nao huko Louisville, kwenye Jumba la mikutano la Ukumbusho. Naye alishangaa sana kuona yale yaliyotukia, ndipo akajaribu kumwambia baba yake kuyahusu.

32 Yeye akasema, "Ni saikolojia tu. Hao watu ni wagonjwa tu kadiri walivyowahi kuwa." Na kwa hiyo—kwa hiyo yeye asingeweza kuamini Hilo.

33 Hatimaye akatoka kanisani, akaolewa na mvulana kutoka seminari ya Kibaptisti, na huyo hatimaye akaiacha imani yake. Yeye alikuwa amefunzwa kuwa mhudumu, na kwa kuwa Wabaptisti hufanya namna hiyo. Na kwa hiyo wao . . . Hatimaye akaondoka, hakutaka kuhubiri. Nao wakahamia kwenda kwa watu wake huko Rockford, Illinois.

34 Hatimaye yeye, Jean, akaanza kuwa na tatizo la wanawake. Akamwendea baba yake akafanyiwe uchunguzi, akarudi Louisville akafanyiwe uchunguzi. Basi, walipofanya hivyo, wakapata kinachoitwa "kivimbe cha kahawia," kiko kwenye tezi za kike. Akikitoa hicho, baba yake, pamoja na upasuaji mkubwa, basi hapana shaka alimwaga ki—kivimbe kidogo ndani yake. Ndipo hatimaye . . . Nao wakamfanyia Eksi-rei ya kilindi na—na matibabu.

35 Na kwa hiyo basi wakati wao . . . aliporudi nyumbani, na akaendelea kuwa na shida.

36 Yapata mwaka mmoja baadaye wakamrudisha akafanyiwe uchunguzi mwingine, nao wakamfanyia upasuaji mkamilifu wa kuondoa mji wa mimba. Basi walipokuwa wakifanya hivyo, baba yake, pamoja na Daktari Humes, ambaye ni mmoja wa madaktari wakuu wa Kusini, wakamfanyia upasuaji, nao ulikuwa umeenea sana, hiyo kansa ilikuwa tayari imeuzunguka utumbo mpana. Basi wakamwacha hapo kitambo kidogo. Ndipo akajaribu matibabu ya eksi-rei tena, nao wakaona

haikufaa kitu, kwa hiyo wakamrudisha tu hospitalini apate. . . Wasingeweza kumpa tena haluli kufanya apate choo, kwa hiyo wakajaribu kumwosha kwa enema. Basi hiyo ikazuia maji yasiingie tumboni tena.

37 Kwa hiyo basi mumewe kidogo alikuwa ni mmoja wa wakosoaji wangu. Basi hatimaye siku moja akashuka kule na kuchukua kitabu akaanza kukisoma. (Basi mwanangu hapa na Ndugu Sothmann, yeye ni mmoja wa wadhamini, yuko hapa mahali fulani.) Basi alikaa tu kwenye vipandio vya kanisa, mbona, kwa yapata siku kadhaa, mpaka . . . Ni—nilikuwa mbali katika mkutano. Niliporudi ni—nilienda kumwona. Basi akaniambia, kasema, "Sasa, yeye hajui ana kansa." Kasema, "Nenda tu ukazungumze naye na kuomba pamoja naye."

38 Basi nilipomwona, yeye alisema, "Ndugu Branham," kasema, "mume wangu atakubali uponyaji wa Kiungu," kasema, "maana nisingeweza kumfanya aangalie kimoja cha vile vitabu, sasa yeye hunisomea ukurasa baada ya ukurasa kila siku, kimoja cha vile vitabu."

39 Kisha nikasema, "Ninaelewa hilo, Jean." Kisha nikasema, "Sasa, Jean, hebu tuzungumze tuone yale Bwana atakayosema." Hakuna mtu chumbani, nesi alijiondoa. Na kwa hiyo tukazungumza kidogo, na baada ya kitambo kidogo likatokea ono. Mimi . . . Yeye yuna kama umri wa miaka arobaini, hajaingia mvi bado, bali alikuwa mzee zaidi na mwenye mvi. Nikasema, "Jean, sasa, umekuwa kwenye mikutano."

"Naam, Ndugu Branham."

40 Nikasema, "Wamekuficha, na kuniambia nisiseme, bali una kansa." Kisha nikasema, "Baba yako na . . . Ama mume wako alisema, 'Usiseme chochote juu yake.' Bali una kansa, Jean. Lakini, sasa, ninataka kukwambia, kwa sababu umekuwa kwenye mikutano. Ono kamwe halijawahi kushindwa. Sasa nitakwambia, Jean, ni BWANA ASEMA HIVI! Unaona?" Unaona?

41 Sasa, unapaswa kuwa na hakika kabisa na hilo, unaona, ya kwamba ninii . . . kwamba ni Bwana. Si dhana; *unaliona*. Unaona?

Na kisha nikasema, "Utaishi. Wao ni . . . Yeye . . . "

42 Akasema, "Ndugu Branham, nilishuku hilo wakati wote." Kisha akasema, "Kwa kuwa nililelewa kwenye makazi ambapo baba yangu ni daktari," kasema, "Ni—ni—nilishuku hilo." Kasema, "Niliwazia hilo wakati wote, hiyo tu ndiyo ilikuwa." Tukaomba.

43 Kesho yake, siku ya pili baada ya hapo, walikuwa wampeleke akafanyiwe upasuaji wa utumbo mpana. Hiyo ni kusema, mwajua, wanakata utumbo na kuweka kijifuko pembeni kisha mgonjwa ananinii tu . . . mpaka watakapokufa, kansa hatimaye

inawaua, anajisaidia kwenye kijifuko. Basi walipokuwa tu wamemwandaa, na tayari ametayarishwa na tayari kupelekwa kwenye meza ya upasuaji, alihisi kabisa hali isiyo ya kawaida. Nao. . .akamwita nesi aje amsaidie kwenda m—msalani. Basi, alipofanya hivyo, alijisaidia vizuri sana kama kawaida. Naye mu—mumewe kamwe asingeweza kujizuia juu yake. Basi kesho yake. . .Hawakumpeleka. Siku ya pili, kawaida, mara tu baada ya kiamshakinywa, akajisaidia tena vizuri sana. Kwa hiyo yeye. . .

44 Daktari wake akapiga simu. Katikati ya kwikwi na kulia, alisema, "Kamwe siwezi kuelewa, hata hatuwezi kupata dalili moja yake hata kidogo. Imetoweka."

45 Sasa, sasa, dada zangu wa thamani, sina sababu ya kusimama hapa kama mtumishi wa Kristo na kusema jambo lisilo kweli, kwa sababu nitahukumiwa kwenye siku ile, na kutupwa nje, kama mnafiki.

46 Sasa, huku Neno la Mungu limefunguliwa, sikumwombea Jean kwa uaminifu zaidi ya nilivyowaombea ninyi, mnaona. Tulielekea tu kwenye maskini kituo hicho kidogo, tukijua ya kwamba maombi ya imani yalikuwa yameombwa. Hilo latosha papo hapo. Neno la Mungu lilisema hivyo, mnaona, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo."

47 Sasa, Mungu yeye yule aliyemponya binti wa Daktari Dyer, ambaye ni Jean. . .Sijui jina lake ni lipi sasa. Lakini mtu huyo hakika ameikumbatia Injili yote. Yale mahubiri ya mwisho kanisani, huyu hapa ameketi pamoja nasi pale pale akisikiliza kwa makini sana, akila ushirika pamoja nasi, na kila kitu kingine, mwanafunzi wa Kibaptisti alikuwa amemjia Bwana kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, inaonyesha tu ya kwamba Mungu anadumu Mungu.

48 Naye yule daktari, baba yake, mtu wa kupendeza, bali kamwe hakuwa ameona kitu kama hicho kikitukia.

49 Sasa, Mungu anao wakati kwa ajili ya mambo yote. Na kutokana na kuamini, nyote wawili ni waaminio. Kwa hiyo wakati mwingine mambo haya hutukia kwa manufaa. Mnajua, Biblia ilisema, "Yanatenda kazi kwa wema."

50 Sasa, mnamkumbuka Ayubu, majaribu yake yote? Sasa, huyo hakuwa ni Mungu akimrudi Ayubu, bali ilikuwa ni Mungu akimthibitisha mtumishi Wake. Kwa hiyo yote yalitenda kazi kwa wema, mnaona. Na halafu Kitabu cha Ayubu kiliandikwa kwa ajili ya vizazi vyote, kwa ajili ya ushuhuda. Sasa, Mungu anatenda kazi kwa wema.

51 Kumbukeni tu, nimeomba, kwa moyo wangu wote, maombi ya imani. Ninyi aminini, na hapo, itakuwa hivyo, hivyo ndivyo itakavyokuwa, ya—yatazamieni tu matokeo.

52 Sasa, kuingia moja kwa moja katika u—ujumbe, (wengi wamesimama), ujumbe mdogo kwa ajili ya jioni.

53 Basi—basi kumbukeni tu sasa, kule katika—katika Ramada, kutakuwako na wahubiri wazuri sana kwenye mkutano huu wa Ramada wakati huu, Wafanyabiashara, kwa hiyo ninyi. . . kule chini Ramada. Kwa hiyo nyinyi hakikisheni mtajaribu kuhudhuria mkutano huu. Ndugu Oral Roberts atakuwako kwa ajili ya usiku wa dhifa.

54 Na, sasa, mimi kidogo ni sehemu ndogo ya Tucson, nitaitetea Tucson. Tunao mmoja kule chini, pia, Jumatatu ijayo usiku, kwa hiyo ikitokea uko karibu na pale, vema, wewe shuka uje kule chini pia. Nawe itakubidi . . . huenda mkanivumilia kidogo, maana ninakusudiwa kuuhubiri huo. Kwa hiyo nyinyi shukeni mje mkiweza Jumanne ijayo . . . Jumatatu ijayo usiku kwenye Moteli ya Ramada, Hoteli ya Ramada, huko Tucson. Na, hakika, sote tunajua kwamba Phoenix ni kitongoji tu cha Tucson. Sote tunajua hilo, mnaona, kwa hiyo—kwa hiyo shukeni mje mwone jinsi watu wa milimani wanavyoishi.

55 Sasa hebu tufungue Biblia zetu katika Zekaria 14, mlango wa 6 na wa 7, ningependa kusoma kwa ajili ya . . . kutoa kutoka hapa muktadha kidogo wa somo ninalotaka kuchukua.

> *Tena itakuwa katika siku hiyo, ya kwamba nuru yake haitakuwa na mwangaza na kiwi:*
>
> *Lakini itakuwa siku moja iliyojulikana na Bwana; si mchana, wala usiku; lakini itakuwa ya kwamba* katika *wakati wa jioni kutakuwako nuru.*

56 Sasa ningependa kutoa kutoka kwenye hili, *Mjumbe Wa Jioni*, kwa ajili ya muk- . . . kwa ajili ya somo: *Mjumbe Wa Jioni*. Hakika, tunaweza kuwa na wajumbe kote katika siku, na kumekuwako na wajumbe siku hii yote ambao Yeye amenena habari zake, lakini unakuja Ujumbe wa jioni. Nasi tunataka kuliangalia hilo usiku wa leo na kidogo kwa njia kama shule ya Jumapili, tulizungumzie kitambo kidogo.

57 Sasa, sote tunajua yale Zakaria hapa alikuwa akizungumzia, kwa sababu kwamba alisema, "Itakuja siku itakayojulikana kwa Bwana, si mchana wala usiku; lakini wakati wa jioni kutakuwako Nuru." Sasa, kama tulijua kwamba haikuwa mchana wala usiku, ingepaswa kuwa ni siku ya—ya—ya utusitusi, kwa namna fulani siku yenye ukungu.

58 Nasi sote tunajua kwamba ustaarabu umesafiri kutoka mashariki ukaenda magharibi. Ustaarabu wa kale kuliko wote tulio nao ni Uchina. Nao ustaarabu umesafiri kutoka mashariki kwenda magharibi, kwa sababu umelifuata jua, na sasa tumeenda kote hadi kwenye Pwani ya Magharibi. Kama tukienda mbele zaidi, tumerudi Mashariki tena, mnaona. Kwa hiyo tuko kwenye mwisho wa safari.

59 Tunaamini, kama Kanisa, kwamba Injili karibu imekamilika. Tunaamini ya kwamba wale wajumbe mashuhuri kote katika nyakati wamekuwa, katika siku hizi za mwisho, mamia kadhaa ya miaka iliyopita, wameyapigania mambo haya makuu; kuhesabiwa haki kwa imani, Luther; utakaso, kwa Wesley; ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa Wapentekoste. Tunaamini ya kwamba elementi hizo zinajumuika kuufanya mwili mkamilifu, kama wa kawaida na wa kiroho.

60 Mtoto mchanga anapozaliwa kawaida, kitu cha kwanza ni kipi? Kitu cha kwanza kinachotoka, ni maji; kitu cha pili, ni damu; na kinachofuata, ni uhai.

61 Yohana wa kwanza 5:7 ilisema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni, Baba, Neno, na Roho Mtakatifu: na hawa watatu ni mmoja." Hao *ni* Mmoja; huwezi kuwa na Baba pasipo kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu. Mnaona, hao ni Mmoja. "Lakini wako watatu washuhudiao duniani, maji, damu, na Roho: nao wanapatana kwa habari moja." Wao si mmoja, bali *wanapatana* kwa habari moja. Mnaona?

62 Sasa, unaweza kuhesabiwa haki pasipo kutakaswa; unaweza kutakaswa pasipo kuwa na Roho Mtakatifu. Unaona? Roho Mtakatifu ni Uwepo wa nguvu za Kristo unaoishi ndani, katika Roho. Sasa, tunaona kwamba ya kawaida ni mfano wa ya kiroho, kwa hiyo Kanisa liko katika upevu wake mkamilifu sasa: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ndio kwanza tumalize zile Nyakati Saba za Kanisa, huko nyumbani, tukizilinganisha hizo vizuri sana.

63 Na, jambo lingine, hivi kuna mtu amewahi kusikia hizo kanda juu ya nyakati za kanisa? Kwenye wakati wa mwisho nilipozichora nyakati hizo pale ubaoni, naye Baba wa Mbinguni anajua hii ni kweli, nilipozikamilisha vizuri nilivyoweza, chini ya uvuvio ambao Mungu angeweza kunipa, Malaika yule wa Bwana mnayemwona kwenye ile picha (wengi wameiona hiyo picha, sivyo, ile Nuru?), alishuka moja kwa moja chumbani, mbele ya watu yapata mia tatu ama mia nne, akaenda moja kwa moja ukutani (kama Nuru namna hiyo) akazichora hizo nyakati za kanisa Mwenyewe. Sote tulisimama hapo tukimwangalia Huyo, tukamwangalia akichora wakati wa kwanza wa kanisa, wa pili, wa tatu, na wa nne, wa tano, wa sita, na wa saba.

64 Sasa, kunao watu wanaoketi hapa ambao ni shahidi wa hayo. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Biblia ilisema, "Katika kinywa cha mashahidi wawili au watatu."

65 Kila mtu ameketi pale, wakishangilia na kila kitu kingine, nikasema, "Pale! Sasa, mmetamani kumwona Huyo, kila mtu anaweza kumwangalia Huyo moja kwa moja." Saa tano mchana, amesimama pale pale ukutani, na kuzichora hizo nyakati za kanisa, kwamba tu ni kiasi gani cha Roho, na halafu giza

kuonyesha ya kwamba Roho alisongwa akatoka na kupitia kwenye Wakati wa Giza kisha akashuka moja kwa moja tena, jinsi tu nilivyokuwa nimezichora. Nasi tunazo, picha zake, na kila kitu kimechorwa, zimening'inia ukutani. Naye huyo hapo kikamilifu. Hapana shaka kwamba Roho wa Bwana aliridhika ya kwamba hizo zilikamilishwa, maana Yeye alirejea na kuthibitisha kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

66 Nasi tunaishi katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati wa kanisa tajiri linalofikiri hawana haja ya kitu, wala hawajui kwamba ni uchi, wenye mashaka, vipofu; nao hawajui, mnaona. Sasa, hizo zote, zikifananisha.

67 Sasa, jua lile lile linaloangaza kwenye. . .linalochomoza Mashariki ndilo jua lile lile linalotua Magharibi. Sasa, hebu tusimame tu kwa dakika moja kuuwekea ujumbe huu msingi. Tunajua kwamba jua, hilo ni j-u-a, mfumo wa jua. Lakini M-w-a-n-a wa Mungu alishuka, katika mng'aro wa Mungu na Nuru ya Mungu, huko Mashariki. Nasi tumekuwa na miaka elfu mbili sasa, iliyowaziwa na Bwana, Yeye alisema, "Ungekuwa ni wakati ambao ungekuwa si mchana wala usiku, kwa namna fulani siku yenye utusitusi; lakini wakati wa jioni kutakuwa Nuru."

68 Sasa, kama mkiangalia, Roho Mtakatifu alishuka juu ya watu wa Mashariki kwanza. Kisha tumekuwa na wakati wa kujiunga tu na kanisa na miisho midogo ya kuokotwa, na kanuni ndogo za kupiganiwa. Lakini basi wakati wa jioni, kwenye eneo la Magharibi, itakuwa Nuru. Nasi tuko kwenye wakati huo sasa! Ustaarabu umekuja kama mwatuko mkubwa kutoka Mashariki, ukiokota dhambi wakati wote kadiri unavyokuja, nao umefikia Pwani ya Magharibi kama kizuizi cha sauti, na umerudi nyuma, napo mahali potovu kuliko pote nipajuapo ni Pwani ya Magharibi. Chochote unachotaka kuwazia, wanacho, dhambi, upotovu, talaka, kuoa, Hollywood, shimo lenyewe la kuzimu! Hiyo ni kweli kabisa.

69 Ninaamini katika utakatifu halisi wa Biblia. Na mimi siamini katika upotovu huu na uozo unaoweka mfano mbele ya watu wetu, unaoitwa Hollywood. Nami daima nimeupinga. Nami nafikiri mtu aliye na Roho wa Mungu ndani yake angeupinga, kwa sababu Roho wa Mungu angeshuhudia "ni makosa" kwake.

70 Sasa nafikiri huo ni mmoja wa. . .Tulikuwa tukienda Paris kuchukua mitindo uchi tupate kuwavua wanawake wetu nguo, sasa Paris huja huku kuchukua yetu. Mnaona? Hollywood inaongoza ulimwengu. Na mitindo uchi tuliyo nayo ya siku hizi, imeshinda ya Ufaransa (wazia tu hilo!), mahali hapo pa ulevi, ugomvi, upotovu wa maadili, na hata hivyo Hollywood inaishinda hiyo kwa jumla.

71 Na televisheni zetu zote, kila kitu walicho nacho ndani yake hakijakaguliwa, mizaha michafu tu, na upotovu uliooza,

imegaagaa ikaingia tu katika kila kitu. Nao watu, ibilisi... Wasingeturuhusu tuwatume watoto wetu kwenye—kwenye sinema miaka mingi iliyopita, sisi Wapentekoste wa mwanzoni, lakini sasa ibilisi alipenyeza moja huku na kuiweka moja kwa moja juu yetu nyumbani. Mnaona? Kwa hiyo aliingiza sinema ndani moja kwa moja.

72 Sasa, na ni—ni kitu cha—cha kuchukiza sana ku—kuwazia ya kwamba ulimwengu umeingia katika upotovu huu, kwa sababu uhuni wote, mnaona, basi ulielea tu huku, ukiambatana na ustaarabu.

73 Lakini wakati wote...nitahubiri moja ya siku hizi, Bwana akipenda, katika siku chache, juu ya *Kuhesabu Kinyumenyume*. Mwajua, na—natumai mnazunguka, na kwa hivyo tu—tunaona tu pale yale yanayotukia. Mungu ameweza kufanikisha jambo fulani na Kanisa Lake, pia, wakati wote, mnaona, wakati mambo haya yakiendelea. Na sasa tuko katika wakati wa mwisho, Bwana ashukuriwe!

74 Kila wakati umekuwa na ujumbe wake na mjumbe. Mungu amelihakikisha hilo. Kila...Hata katika nyakati za kanisa, tunaona ya kwamba kila mmoja ulikuwa na mjumbe, na kila mmoja uliishia wakati wake; na mwingine ukaja, nao huo ukaondoka; kisha mwingine ukaingia; na kuendelea hata kwenye wakati wa saba wa kanisa; kila nyota, kila malaika wa kanisa, kila mjumbe.

75 Nasi tunaona ya kwamba, kwenye wakati wa mwisho wa kanisa, katika Ufunuo 10, kutakuwako na baragumu itakayolia, na kulikuwako na sauti saba zilizotolewa kwenye... Wao hawakuruhusiwa kuandika. Bali ulitiwa muhuri upande wa nyuma wa kile Kitabu, ile mihuri saba ilikuwa upande wa nyuma ya kile Kitabu. Kitabu kikiisha kuandikwa, basi kinatiwa muhuri huko nyuma kwa mihuri saba. Sasa, hakuna mtu anayejua kwamba hiyo ni nini. Lakini Hicho kilisema, "Katika siku za malaika wa saba atakapokuwa akiutangaza Ujumbe wake," huyo ni malaika wa *duniani*, sasa.

76 Kwa sababu Malaika *huyu* alishuka kutoka Mbinguni; naye *huyu* alikuwa duniani; *malaika* ni "mjumbe," mjumbe kwa wakati.

77 Halafu tunaona ya kwamba Yeye aliweka ninii Yake... alikuwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake kisha akainua mkono Wake na kuapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, kwamba hapatakuwa na wakati tena (wakati hizi sauti saba zilipotoa sauti, ngurumo saba zilitoa sauti zao). Naye akawaambia, "Usiandike, bali kitie muhuri." Nasi tuliona ilikuwa ni upande wa nyuma ya hicho Kitabu.

78 "Lakini wakati malaika wa saba alipokuwa ameumaliza Ujumbe wake, kutabiri kwake kwa siku hizo, basi siri ya Mungu inapaswa kutimizwa," kila mtu anajua ya kwamba Biblia

inasema hivyo. "Siri ya Mungu, kwamba Mungu ni nini, Mungu ni Nani, na yote kuhusu njia ya kuingia kwenye ubatizo na kadhalika, hayo yanapaswa kutatuliwa yote katika siku hiyo."

79 Kila mjumbe amekuwa na ujumbe wake, na u—ujumbe na mjumbe wa wakati huo. Na ni ajabu mno kwamba kila mjumbe. . .Hata tuliona katika nyakati za kanisa (na usiku wa leo tutarejea kwenye Agano la Kale na kuona kwamba ni jambo lile lile) kwamba Mungu humtuma mjumbe wa wakati huo mwishoni mwa huo wakati; sikuzote mwishoni, si mwanzoni kamwe. Mwishoni!

80 Sasa, wakati wa Luther ulipofifia, ndipo akaja Wesley. Ndipo wakati utakaso wa Wesley ulipofifia, wakati wa Pentekoste ukaingia. Mnaona? Sikuzote ni mjumbe anaufungua ujumbe mpya mwishoni mwa ule wa zamani. Hilo limefanyika katika kila wakati. Tunajua hilo kwamba ni kweli.

81 Hili limerudiwa kila wakati kote katika Biblia. Tunaona hilo katika Maandiko matakatifu, kote kote, ya kwamba mwishoni tu mwa wakati wa zamani na ule mpya ukiingia, wakati huo hufifia na wakati mpya unaingia, Mungu humtuma mjumbe.

82 Na kama kawaida—kawaida, kila wakati mjumbe anapokuja, daima ni wito wa kurudi kwenye Neno, haushindwi. Kumbukeni, Huu ndio ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, hapawezi kuwa na lolote linaloongezwa Kwake au kuondolewa Kwake. Ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Na njia pekee tunayoweza kuwa na hakika: kama kitu chochote kikiinuka miongoni mwetu ambacho ni kinyume na ufunuo huu, basi ni cha uongo. Mnaona? "Vurumisha urejee kwenye Neno!" Na sikuzote kuwaita warudi.

83 Na katika kila kisa katika Maandiko, kila kisa, Mungu humtumia nabii kuuita wakati huo urudi, sikuzote. Hakuna mfa-. . .La, halijashindwa hata wakati mmoja, Yeye daima humtuma na—nabii! Na sasa kwa nini Yeye hufanya hivyo? Ni kwa sababu Biblia inasema, "Nabii ndiye anayejiliwa na Neno la Mungu," mfunuzi wa Neno.

84 Sasa, na—na—natumaini ya kwamba sieleweki vibaya. Mnaona? Sikusudii kueleweka vibaya, bali ninakusudia kuwa mkweli na mwaminifu kwa ule wito. Tunataka kuwa hivyo.

85 Sasa, Mungu daima humtumia na—nabii, mwanadamu. Ukilitumia kundi la watu, unapata mawazo tofauti tofauti; mnaona, kila mtu, watu wawili. Kamwe hajawahi kuwa na manabii wawili wakuu duniani kwa wakati mmoja. Yeye humchukua mmoja, kusudi huyo mwingine apachukue mahali pake kwa ajili ya siku nyingine, ujumbe mwingine. Kamwe hawi na wawili, Yeye ana mmoja kwa wakati mmoja.

86 Na Mungu asiye na kikomo kamwe habadilishi ratiba Yake, Yeye hana budi daima kudumu na kile alichoanza nacho. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kuwa na imani katika yale anayosema,

Yeye hawezi kubadilika. Kama alimwokoa mtu juu ya msingi wa imani yake katika Mungu, mtu wa pili hana budi kuokolewa kwa njia hiyo hiyo.

87 Wakati Mungu alipofanya mahali ambapo Yeye angeweza kushiriki pamoja na kiumbe Chake, Adamu alijaribu kujitengenezea njia mwenyewe, ndipo akashona majani ya mtini kwa ajili yake na mkewe, kutengeneza nguo. Mungu alizikataa. Basi Mungu akaamua ni juu ya ratiba ama msingi gani ambapo Yeye angekutana na mwanadamu na kushirikiana naye, na hiyo ilikuwa ni damu iliyomwagika. Na kamwe hajaibadilisha.

88 Sasa, kama Methodisti kwa Baptisti, tunaweza kusalimiana kwa mikono. Lakini juu ya msingi kati ya Methodisti na Baptisti hatuna vitu shirika, mimi ninaitetea Baptisti nawe unaitetea Methodisti, au vinginevyo. Lakini kuna msingi mmoja ambapo waaminio wote wanaweza kukutania, hapo ni chini ya Damu iliyomwagika. Hapo ndipo tunapokutana na kuweka kando mambo haya yote. Kwa hiyo sote hatuwezi kuingia katika dhehebu moja, hatuwezi kufanya hivyo.

89 Madhehebu haya madogo, nafikiri Mungu amekuwa ndani yao, kitu hicho chote. Lakini watu. . .maana sisi ni tofauti. Kila mtu huona tofauti, kila mtu huona tofauti, hakuna akili mbili zilizo sawa kabisa. Hakuna watu wawili walio sawa kikamilifu, wanadai; hakuna pua mbili, hakuna alama mbili za vidole. Mnaona, tumefanywa tofauti, hivyo tunapaswa kuwa na makundi tofauti.

90 Bali Mungu daima hutenda kazi na mtu binafsi. Yeye hakuokoi kwa sababu wewe ni Mmethodisti; Yeye hakuokoi kwa sababu wewe ni Mbaptisti; Hakuokoi kwa sababu wewe ni Mpentekoste. Anakuokoa kwa sababu Yeye amekushughulikia *wewe* binafsi! Nawe unaokolewa juu ya msingi huo, kwamba umelikubali. Kwa hiyo basi, Mungu, kukushughulikia, Yeye hakushughulikii kulingana na utaratibu wa kanisa Lake, Yeye hukushughulikia kama mtu binafsi.

91 Kwa hiyo wakati Mungu alipowatuma manabii Wake, wajumbe Wake wa Agano, Yeye alinena na mtu mmoja, naye mtu huyo ilimbidi kuleta Ujumbe. Wengine walitoka kwake, kila mahali, wakiuleta Ujumbe ule ule. Lakini kulipaswa kuwe na makao makuu moja. Mungu daima amekuwa nayo. Ninashukuru Yeye anayo usiku wa leo; hayo ni Roho Mtakatifu, hakika, sote tunajua. Sasa, si kundi fulani, bali Roho Mtakatifu ndiye Makao Makuu ya Mungu. Huyo ndiye Mjumbe wa Mungu wa wakati huu.

92 Sasa, kwa kuwa ni, kwa nabii ambaye Neno sikuzote linamjilia, kama wao ni nabii wa kweli wa Neno, Mungu huthibitisha Neno Lake kwa nabii huyo.

93 Sasa, kumekuwako na manabii wengi wa uongo, tumekuwa nao kote katika nyakati. Tukirudi kwenye Agano la Kale,

tunawaona wakiinuka na kunena katika Jina la Bwana, na ilikuwa—haikuwa sahihi. Mungu asingeshughulika nalo. Kamwe Yeye hathibitishi chochote ila Neno Lake Mwenyewe. Kwa vyovyote vile, Yeye asingeziendesha shughuli Zake namna hiyo. Mnaona?

94 Ninyi kumbukeni tu, Mungu huthibitisha Neno Lake pekee! Na nabii wa kweli pekee ndiye. . .Na njia pekee unayoweza kujua kama yeye ni wa kweli ama siye, ni kwa Neno. Hiyo ndiyo njia ya kumhukumu.

95 Sasa kama ukiangalia, kama katika zile siku ambapo—ambapo Mikaya, pale walisimama manabii mia nne wa Kiebrania, mbele ya Ahabu na Yehoshafati, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, 'Kwea ukafanikiwe.'" Kimsingi walikuwa sahihi. Ndipo Mikaya akaitwa jukwaani, yule ambaye wote walimchukia. Sasa, ilionekana kana kwamba ikiwa . . . Mia nne (Si—simaanishi manabii wa Baalim) Manabii wa Kiebrania walisimama kwa moyo mmoja, na kusema, "Kwea Ramothi-gileadi, Bwana atakubariki na kukufanikisha." Nao hao watu hawakuwa ni wanafiki, walikuwa wamevuviwa kabisa! Bali ninii yao . . .

96 Basi kwa nini maskini jamaa huyu mmoja a—aitwae Mikaya aje, ambaye alikuwa ni mwana wa Imla, na kurudi na kutabiri kinyume chao? Sasa, hiyo ilihitaji ushupavu, ilihitaji imani. Mnaona? Lakini alijuaje ya kwamba alikuwa sahihi? Kama ungalikuwa umesimama pale, ungejuaje? Njia pekee unayoweza kufanya, ni kuchukua yale huyo mtu asemayo na kuyalinganisha na Neno. Mnaona? Sasa, Mikaya alikuwa moja kwa moja kwenye Neno, kwa sababu Eliya, yule nabii mashuhuri aliyekuwa na Neno la Bwana, alikuwa ndio kwanza tu amemlaani Ahabu na Yezebeli na wote. Mnaona? Basi Mungu angewezaje kugeuka na kubariki kile laana ilikuwa juu yake? Mnaona, kwa hiyo isingewezekana kabisa.

97 Sasa, tunaona ya kwamba Mungu huthibitisha Neno Lake. Neno la nabii, kama yeye ni nabii, basi ni . . . yeye ananena kulingana na Neno. Biblia ilisema katika mahali pamoja, ikasema, "Wasiponena kulingana na torati na manabii, hakuna Nuru ndani yao." Kisha kuita . . . Ndipo mjumbe huyu anawaita Walioitwa watoke. Yeye yuko moja kwa moja na Neno la Mungu, inathibitisha kwamba yeye ni sahihi.

Angalieni, angalieni, sasa tutawaita watu wachache na kusikiliza.

98 Nuhu alikuwa shahidi wa Mungu kwa ajili ya wakati wa mwisho ule uliotangulia gharika. Sasa, angalieni jinsi ujumbe wake ulivyokuwa ni kinyume cha ulimwengu wote uliotangulia gharika. Mbona, mtu huyo alichukuliwa kuwa mwendawazimu. Mbona, ninii yake . . . Lakini, hata hivyo, yeye alikuwa hasa na Neno la Bwana. Sasa, Mungu alikuwa amesema

Yeye "asingeweza kuvumilia dhambi," kwa hiyo Yeye... watu walipoanza kutenda dhambi, ndipo Mungu akashuka naye Nuhu akahubiri ujumbe wa wakati wa mwisho. Ilikuwa ni wakati gani? Kabla tu ya wakati wa mwisho, mjumbe huyu aliinuka. Mungu alimtuma nabii huyu pamoja na ujumbe kwa ajili ya wakati wa mwisho. Naye alichekwa, akadhihakiwa, akafanyiwa mzaha, na ni wokovu wa nyumba yake pekee aliowaokoa. Hiyo ni kweli. Hakuna mtu aliyeweza kumwamini. Lakini alikuwa na ujumbe wa wakati wa mwisho. Sasa, wote wasioamini walihukumiwa, nao waliouamini huo ujumbe waliokolewa. Mungu aliwapa Uzima nao waliokolewa, na wale ambao hawakuuamini Huo walipotea.

99 Sasa, ninafananisha kitu fulani. Mwangalieni Mungu, jinsi amefanya hili mara tatu.

100 Na tatu ni namba kamilifu ya Mungu. Mungu hukamilika katika tatu, kama vile, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na "kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu." Yeye anakamilika, maana *tatu ni* "ukamilifu" Wake. *Tano ni* namba ya "neema." Saba ni... Namba ya "ibada," *kumi na mbili*. *Arobaini ni* namba ya—ya "mateso." Na *hamsini* ni "yubile," ibada. "Pentekoste" inamaanisha *hamsini*. Na, siku arobaini Musa alijaribiwa, siku arobaini Kristo alijaribiwa, mnaona. Na mifano hiyo yote. Sasa, Mungu hukamilika katika tatu.

101 Kunayo maangamizi matatu. Moja, wakati Nuhu alipoingia *ndani ya* safina; mara ya pili, Lutu *akatoka* So—Sodoma. Angalia, Yesu alirejea hizo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Tazama! Mmoja aliingia *ndani*, huyo mwingine *akatoka*, na anayefuata anapaa *juu*. Uh-huh. Mnaona? Uh-huh. Anaingia *ndani*, *anatoka*, anapaa *juu*! Sasa, huo ndio utaratibu wa Bwana. Mnaona, Yesu aliwarejea manabii hao wawili. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu," mnaona, "na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," Ibrahimu akiwa ni nabii, "kama ilivyokuwa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Mnaona, akiwarejea hao.

102 Sasa, Musa, nabii mwingine, mwishoni mwa wakati wa Kimisri. Tunaona ya kwamba wakati Mungu alipokuwa akienda kuwakomboa watu Wake, nao Wamisri walikuwa wamewatesa sana, na kuweka wasimamizi juu yao, wasimamizi juu yao, hasa. Na kwa hiyo basi kabla tu ya maangamizi yao, Mungu, kama sikuzote, Yeye alimtuma nabii akiwa na Neno la Bwana. Kumbukeni, nabii alikuwa akithibitisha yale hasa Mungu (mamia ya miaka kabla ya hapo, miaka mia nne na kitu kabla ya hapo) alikuwa amemwahidi Ibrahimu, ya kwamba uzao wake ungekuwa mgeni katika nchi ya kigeni, bali Yeye angewatoa kwa mkono wenye nguvu. Mwajua, kwenye kichaka kilichowaka moto wakati Musa alipokutana na Mungu, na

Yeye akamwambia, "Nimesikia kilio cha watu Wangu, nimeona mateso yao, na ninakumbuka agano Langu." Kulikumbuka Neno Lake!

103 Kumbukeni, Yeye angali analikumbuka Neno Lake! Mnaona? Hashindwi, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile kila wakati. Sababu ya mimi kusema mambo haya, ni kusudi tuweze kuyaweka niani mwenu na kutafakari. Hata ninyi watu ambao mmekuwa wagonjwa; mliona nilisema "mmekuwa" wagonjwa.

104 Sasa, angalieni sasa, nyinyi watu nyote inawapasa kukumbuka jambo hili, kwamba Mungu hawezi kubadilika! Yeye ni Mungu asiyebadilika. Nyakati hubadilika, watu hubadilika. Mungu hana kikomo, Yeye hawezi kubadilika! Ninii Yake. . .Hana budi kudumu yeye yule jana, leo, na hata milele, hana budi kubaki daima. Na kama tunaamini Hili kuwa ni Neno la Mungu, tunaweza kuweka imani yetu juu ya kitu chochote Yeye alichosema. Mnaona?

105 Sasa, mnaona hapo vile ujumbe Wake huja, jinsi Yeye hutuma ujumbe Wake. Hawezi kubadilisha hilo, daima amefanya hivyo. Yeye hana budi sikuzote kubaki vivyo hivyo. Hivyo ndivyo atakavyofanya daima. Sasa, kumbukeni, Yeye anafanya hivyo wakati gani? Kabla tu ya maangamizi, mwishoni tu mwa wakati. Hapo ndipo Yeye anapoutuma ujumbe Wake kuwaita watu Wake watoke, (daima wanawafanya kuchanganyikiwa), nao hawa hapa wanakuja.

106 Sasa, katika siku za Musa, waaminio waliokolewa, wasioamini wakaangamia.

107 Wale walioamini ujumbe wa Musa kutoka kwa Mungu, sasa, wasingaliweza kufanya hivyo isipokuwa Musa awe ni nabii aliyethibitishwa na Mungu na kuthibitisha ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa pamoja naye. Hilo lilimfanya nabii. Alifika huko nje na kusema, "Kesho, wakati kama huu, mtaona jambo *fulani-na-fulani* likitukia." Kesho, likatukia. Hivyo tu. Nabii yeyote wa kweli wa Mungu anayenena katika Jina la Bwana atafanya hivyo. "Na itakuwa ya kwamba jambo *fulani-na-fulani* litatukia. Ninapanda kwenda kwa Farao, lakini yeye atakuwa mgumu, atakuwa na moyo mgumu. Atasema atatuacha twende bali hatafanya hivyo." Ndipo, likatimia. Mnaona? Kwa nini? Basi watu walijua mtu huyu alitumwa kutoka kwa Mungu. Na ndipo wakaanza kuona ya kwamba Mungu alimbariki, nao wakamheshimu na, walipomheshimu, mambo makuu yakatukia.

108 Nao watu waliocheka na kudhihaki wala wasingeukubali ujumbe wake, waliangamia pamoja na wasioamini wengine.

109 Lakini waaminio walitoka wakaingia kwenye nchi ya ahadi, walienda chini ya ujumbe uliotiwa mafuta wa yule mjumbe. Ulikuwa ni ujumbe wa ukombozi, ambao Mungu aliahidi Yeye angewaleta watu Wake kwenye nchi iliyojaa maziwa na asali.

Nalo likatukia, kwa sababu Mungu alikuwa tayari amesema hivyo, naye Musa akaja na akathibitishwa kama mjumbe wa siku hiyo.

Sasa, hilo linalileta dhahiri sana kwetu.

110 Vema, ndipo tunaona ya kwamba Musa alitambulishwa vizuri.

111 Ndipo kwenye badiliko la huo wakati, wakati uliwadia kwa. . .kati ya torati na neema. Ilibidi pawe na wakati ambapo Masihi huyu aliyenenwa angekuja. Tunaona ya kwamba wakati ambapo watu walikuwa wameivuruga torati, wakaiweka yote chini ya kundi kubwa la kitu fulani, nao walikuwa na kila namna ya—ya mapokeo ya binadamu, waliyokuwa wameingiza ndani yake. Basi kwenye badiliko la wakati akaja Yesu, Nabii mwingine, Mungu-Nabii.

Sasa, mnasema, "Yeye hakuwa nabii."

112 Biblia ilisema alikuwa hivyo. "Bwana Mungu wenu atamwinua Nabii kama nilivyo mimi." Yeye alikuwa Mungu-Nabii, kwenye lile badiliko la wakati kati ya torati na neema, ambaye alikuwa amenena habari zake kwa miaka hii yote. Baada ya kumpa Musa torati, ndipo kwenye lile badiliko la wakati, wakati aliposema lingetendeka, basi yeye alirejea kwenye neema. Naye akamtuma Nabii akitabiri juu ya huo wakati. Sasa—sasa, waaminio, Yeye aliwakusanya; wasioamini wakaangamia katika siku Yake. Wote waliomwamini Yeye waliokoka; wote ambao hawakuamini ujumbe Wake walipotea.

113 Hilo ndilo hasa lililotukia katika siku za Nuhu; hilo ndilo lililotukia katika siku za Lutu; hilo ndilo lililotukia katika hizo siku zingine, siku za Musa; hilo ndilo lililotukia katika siku za Yesu Kristo. Kwa kuwa waliudharau ule ujumbe wakaangamia, na wale walioamini huo ujumbe wakapotea . . . ama wakaokoka.

114 Sasa, sasa, ndipo kinakuja kile kipindi cha kanisa. Tuliishi huko nyuma katika wakati wa Nuhu, ule uliotangulia gharika; tukaingia katika kipindi cha torati; halafu katika kile kipindi cha wakati wa neema, kanisa. Na sasa kipindi cha wakati wa kanisa kinaisha. Sote tunajua hilo.

115 Sasa, kama Mungu alifanya *hivi-na-hivi* katika kipindi hicho cha wakati, katika vipindi hivyo vingine viwili vya wakati, Yeye hana budi kubaki yeye yule na kufanya vivyo hivyo katika kipindi hiki cha wakati, maana Yeye alisema angefanya hivyo. Nitalithibitisha katika dakika chache, kwa Neno, ya kwamba Yeye alisema angefanya hivyo. Sasa, Yeye hawezi kubadilisha mpango Wake, Yeye ni Mungu. Angalia alilofanya katika vipindi hivyo vya wakati.

116 Sasa tunakuja katika wakati wa mwisho wa vipindi vya wakati wa kanisa. Hilo ndilo nililosoma usiku wa leo:

> Itakuwa Nuru wakati wa jioni.

117 Tumekuwa na nyakati nyingi za kusikitisha, bali kutakuwako Nuru. Mwana yeye yule aliyekuja na kubadilisha kipindi cha wakati wakati huo, anarudi tena! Hiyo itakuwa ni kutoka duniani hadi Utukufuni. Tutaingia katika hilo. Wakati mmoja tuliingia *ndani*, huo wakati mwingine tukatoka *nje*, na wakati huu tunapaa *juu*! Mnaona? Vema: ndani, nje, juu. Tunaelekea kwenye wakati wa mwisho. Na hatuji tu, tumefika tayari. Tuko kwenye wakati wa mwisho!

118 Mungu anapata nini katika wakati huu wa mwisho? Mungu anakuta katika wakati huu wa mwisho yale hasa aliyokuta kwenye nyakati zingine za mwisho, kutokuamini! Daima amekuwa hivyo, Yeye, ajapo, a—anakuta kutokuamini. Anakuta kwamba mpango aliowawekea watu . . .

119 Huko nyuma katika wakati wa Nuhu, kama wangaliishi kwa maagizo Yake, wakatoa dhabihu . . . Waliiacha. Wakati Yeye alipokuja, alikuta hili, kitu hicho kikiendeshwa vibaya.

120 Jambo lile lile Yeye alilofanya wakati alipokuja duniani, Yeye alikuta watu na Mafarisayo, na kadhalika, wakiifuata torati. Wao walikuwa wanafanya nini? Hakuna uaminifu kwake hata kidogo, kuendelea tu na kuichafua kwa maskini njia yoyote, na "Mradi tu walijiunga na kanisa, na hilo ndilo tu walilohitaji." Na hilo ndilo alilokuta.

121 Na hilo ndilo amekuta tena! Yeye anapata kitu kile kile, watu hawabadiliki. Kwa hiyo kama alituma mpango wake nao watu wakakosa kuuamini hapo na wakaangamia, waliuamini na wakaishi, (sasa, juu ya hao wawili), haina budi kuwa vile vile wakati huu. Haina budi kuwa vile vile. Hakuna . . .

122 Sikuzote imekuwa ni vita kwa mjumbe kutenganisha ya kale na yaliyo mapya. Sikuzote imekuwa ni vita hivyo, kwa—kwa mjumbe kuja na kutenganisha ya kale na yaliyo mapya, ingawa sikuzote ujumbe hauna budi kuwa ni wa Kimaandiko, sasa, kwa kuwa kila mmoja amebashiri juu ya huyo mwingine ajaye.

123 Sasa, hebu tuchukue, kwa mfano, Yesu. Jinsi ilivyokuwa vigumu, Yeye kuja na kubadilisha ujumbe kutoka kwa torati hadi kwa neema. Hata hivyo Biblia ilisema ingekuja jinsi hiyo, "Atakuja Ma—Masihi, nayo dhabihu ya kila siku itaondolewa." Nasi tunajua ilitabiriwa kupitia manabii. Lilikuwa ni jambo kubwa jinsi gani Kwake kufanya hivyo. Lakini tunaona ya kwamba Yeye alifanya hivyo. Naye yule . . . Alifanya hivyo kwa sababu Maandiko yalisema, nao waaminio wa siku hiyo (wanaojiita waaminio) kabisa wasingekubaliana na Yeye.

124 Waangalie hao Mafarisayo, Masadukayo, walikuwa na mapokeo yao wenyewe na hakuna mtu atakayewatikisa kutoka kwake. Hilo ndilo waliloamini, mama yao aliamini hilo, baba yao aliamini hilo, na babu yao, nyanya yao aliamini hilo, na "Musa alisema hivyo!" Lakini Musa yule yule aliyetoa torati alikuwa ndiye Musa yule yule aliyesema Jamaa huyu

angekuja, nao wakashindwa kumtambua kwa sababu walikuwa wameliingiza Neno la kweli la Mungu katika mapokeo nao walikuwa wameacha kanuni Zake kuu. Nayo ilibidi iwe hivyo.

125 Angalieni, kila mmoja alitabiri huyo mwingine angekuja. Kila mmoja wa hao wajumbe, baada ya ujumbe, alitabiri angekuja. Sasa, lakini watu sikuzote huuchukua ujumbe wa siku ambao wamekuwa nao, wanauweka.

126 Hebu tulifafanue, kidogo zaidi vizuri, hebu tumwangalie Luther. Wakati Luther alipohubiri kuhesabiwa haki kwa imani, yeye alikuwa ndiye mjumbe, malaika wa wakati huo wa kanisa, vema, wa Wakati wa Kanisa la Sardi. Sasa, angalieni, wakati alipohubiri, aliwaweka Walutheri katika utaratibu. Sasa, basi, huyu hapa Luther akaenda akiutangaza. Ndipo Wesley alipoingia, Wakati wa Kanisa la Filadelfia, akiwa na ujumbe wa utakaso, mbona, ilikuwa ni vigumu kwa Luther kuuona huo. Hao Walutheri wasingeuamini.

127 Ndipo wakati Wesley alipowafanya watulie kabisa kwenye Pilgrim Holiness na Methodisti Huru, na kadhalika, juu ya utakaso, ndipo ukaja ujumbe wa Kipentekoste, mbona, ilikuwa ni vigumu kwa Methodisti kuamini huo. A-ha, hakika, ilikuwa ni vigumu. Mnaona, ni ninii . . .

128 Hata hivyo mmoja ananena juu ya huyo mwingine, tukinena Kimaandiko. Henoko alinena juu ya maangamizi yajayo, kwa kunyakuliwa kwake, Mungu akimpeleka nyumbani; alikuwa ni shahidi. Ibrahimu aliwaambia juu ya Musa. Naye Musa akanena juu ya Masihi. Mnaona, wanaendelea kutangaza, mmoja kwa mwingine. Masihi alinena juu ya wakati huu, akielezea huu utakavyokuwa!

Mnasema, "Aa, Ndugu Branham!"

129 Loo, naam, alieleza! Hebu tuninii tu . . . Ninayo Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa chini, nami nitayarejea tu mawili ama matatu yake. Hebu tuchukue Mathayo 24. Sasa hebu tuchukue Mathayo, mlango wa 24, na tusome yale Yeye aliyowaambia pale yangetukia, jinsi ambavyo "Mataifa yataondoka kupigana na taifa." Lakini, kumbukeni, kisha anafika pale chini na kusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Yeye alitabiri, alitabiri mambo haya yangetukia!

130 Alisema, "Sasa, wakati mambo haya yote yalipokuwa yakitendeka, wakati haujatimia bado," na kadhalika. Lakini kasema, "Jifunzeni mfano wa mtini, wakati ni mchanga na unachipuza matawi, na miti mingine yote, basi mnajua wakati wa kiangazi umekaribia. Vivyo hivyo, myaonapo mambo haya yakitimia, tambueni ya kuwa wakati umekaribia, hata mlangoni." Sasa, mwonapo nini? Mtini ukichipuza, na miti

mingine yote ikianza kuchipuza, ilikuwa ni ishara. Nayo Israeli daima imekuwa ndio mtini.

131 Yoeli hata alitabiri juu yake, "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na parare na kukimaliza kitu hicho. Lakini Mungu aliahidi, 'Nitarudisha, asema Bwana.'" Naye atafanya hivyo. Lakini kabla Yeye hajaurudisha huo katika hali yake ya kiroho, Kanisa la Kimataifa halina budi kuondolewa. Hatakuwa na wawili wao wakati ule ule. Sasa, huwezi kuyafanya Maandiko yajivuruge yenyewe namna hiyo. Unaona? Kamwe hajawahi kuwa na mashahidi wawili wakati ule ule, mashahidi wakuu, wala Yeye kamwe hajawahi kuwa na—Yeye kamwe hajawahi . . . Hana Makanisa mawili wakati ule ule.

132 Tazameni, ni . . . Kanisa la Kimataifa halina budi kuondolewa kwanza, kwa ajili ya Wayahudi, ndipo mwisho wa yale Majuma Sabini ya Danieli unatokea. Ile miaka mitatu na nusu Masihi alitabiri, kisha akakatiliwa mbali, yule Mtawala, katikati ya juma la sabini. Ndipo, basi, kuna majuma matatu na nusu yaliyosalia bado. Nasi tunaona wale manabii wawili wa Ufunuo (Yeye kamwe habadilishi koti Lake tena), wa Ufunuo 11, wanashuka na kuwatabiria Wayahudi. Sasa, Kanisa litaondolewa kwenye wakati huo.

133 Nasi tunawaona Israeli, mara ya kwanza kwa miaka mia kadhaa, karibu zaidi ya miaka elfu mbili, sasa limekuwa ni taifa; jeshi lake lenyewe, pesa zake lenyewe. Israeli wako kwenye nchi ya uenyeji wao; taifa lake lenyewe, bendera yake lenyewe, ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Wao ni taifa! Mbona, ni moja ya ishara kuu sana tungaliweza kuwazia, sasa hivi, Israeli katika nchi ya uenyeji wao. Naye Yesu alisema, "Kizazi hiki kinachoona Israeli ikirudi kwenye nchi ya uenyeji wake hakitapita mpaka hayo yote yatakapotimizwa." Unaona, Yeye alinena juu ya siku hii.

134 Hebu nitoe tu mwingine. Katika Timotheo wa Pili 3, Yeye alinena juu ya kanisa kwenye wakati wa mwisho, kasema, "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Uchukue ulimwengu wa kanisa, wote, "wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu," wanakaa nyumbani na kuangalia kipindi cha televisheni kabla ya kuhudhuria mkutano wa maombi Jumatano usiku.

Unasema, "Hao ni Baptisti."

135 Hao ni Wapentekoste! Hakika! Naam, bwana. Loo! "Wakaidi, wenye kujipenda, wapendao anasa"; ukiliweka Neno moja kwa moja chini ya pua yao, hawataliangalia. A-ha. "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu"; ukiwaambia hao wanawake hawapaswi kuzikata nywele zao, wanazikata kwa vyovyote vile. A-ha. "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiotosheka, na wasiowapenda walio sahihi. Wenye . . . "

Unasema, "Hao ni makafiri." La! La!

136 "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake," Nguvu zinazoweza kuwaokoa na usumbufu huu, mfumo wa ulimwengu wa sasa. "...Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao." Sijali hao watu wengine wanasema nini, ni wewe kama mtu binafsi mbele za Mungu, huna budi kujibu. Haijalishi mwanamke huyu afanyacho au mwanamke yule afanyacho, ama, mwanamume huyu afanyacho au mwanamume yule afanyacho, ama, mhubiri huyu asemacho au mhubiri yule asemacho; ni wewe na Mungu. "Wenye mfano," kuyafuata mapokeo, "bali wakikana Nguvu zake; hao nao mjiepushe nao." Hivi tunaishi katika siku hiyo? Hakika tunaishi!

137 Angalieni tena katika wakati wa mwisho wa kanisa. Roho Mtakatifu, Yesu Mwenyewe, "Mimi Yesu nilimtuma malaika Wangu kuyashuhudia mambo haya." Nao Ufunuo, mlango wa 3, ukinena juu ya wakati huu wa kanisa, Yesu akitoa ushuhuda wa yale yatakayotukia katika siku za mwisho, Yeye alisema, "Kanisa litakuwa tajiri, Laodikia, lenye uvuguvugu," Linaweza kurukaruka vya kutosha wakati muziki unapocheza kupaza sauti. Mnaona? Hiyo ni kweli. Bali kwa ajili ya ushuhuda na maisha yatakayosafika, liko mbali nalo.

138 Sininii...Nisingewaudhi kwa chochote, bali nilikuwa na ono sio muda mrefu uliopita la kuwa katika Paradiso ya Mungu. Siwezi ila kuwaambia Kweli. Mungu, tusaidie sisi wahudumu kuwa waaminifu katika mambo haya na kusema Kweli!

139 Mnaona? "...?...baridi..." Biblia ilisema wangekuwa hivyo, kwa hiyo watakuwa hivyo. Kama lilitimia kikamilifu pamoja na Luther, likatimia kikamilifu pamoja na...katika Wakati wa Filadelfia pamoja na Wesley, halina budi kulinena na kuwa kamilifu...Limelinena, nalo litakuwa hivyo hasa katika Laodikia.

140 "'Tajiri, hawana haja ya kitu!'" Tunaweza kuweka mabilioni ya dola katika mijengo, tunaweza kuweka kila kitu ambacho kila—ambacho kila...burudani za kilimwengu, tunaweza kujenga makanisa yaliyo mazuri kuliko yote. Hiyo ni sawa, hakuna kitu, hiyo ni sawa kabisa.

141 Ila ninajaribu kusema, ndipo wakati Ujumbe unapoanza kupamba moto juu yao, hawakutaki. "Wewe ni mpumbavu! Wewe ni mlokole! Unapaswa kuwa uliishi miaka hamsini iliyopita." Mnaona? Loo, huenda ukawazia kwamba, "Sitakuwa na mchungaji kama huyo." Ni mchungaji wako, haidhuru! Yezebeli kamwe asingekubali kwamba huyo Eliya alikuwa mchungaji wake, bali hakika alikuwa. Bila shaka alikuwa. Alitumwa, mfano, mjumbe wa taifa la Israeli. Na leo hii Roho Mtakatifu wa thamani na Neno la Mungu ni Mjumbe kwa kanisa, kuwanyosha na kuwarudisha kwenye Neno. Tunazungumza juu

Yake, bali huoni yeyote akisogea. A-ha, mnaona, tunayavuruga mambo hayo sana.

142 Nilimsikia mtu fulani, kama katika ushuhuda, akisema, '"Mwinueni juu,' mnamwinuaje juu?" Na, loo, chukueni tu maskini itikadi ndogondogo! Mtu fulani alisema, "'Kesheni mkiomba,' hiyo inamaanisha ufungue jicho moja unapoomba, uangalie kwa hilo lingine. 'Kesheni mkiomba.'" (Mbona, *kesha* linamaanisha "mtazamie kule kuja kwa Bwana," na mwombe sana.) Mnaona, ni kukigeuza tu kitu hicho.

143 Hivyo basi, katika jambo hilo, tufanye nini? Tunajiundia desturi ndogo yetu wenyewe (na halafu kama . . .) kama imeundwa na Mungu ama la. Nasi tunatoka nje, muda si muda mwajua, tunalo kundi dogo linalotufuata sisi, na kuwavuta kutoka kwenye ule mwili wenyewe wa kanisa. Hiyo ni kweli. Badala ya kuingia na kuomba na kulitatua jambo hilo, na kuuacha huo mwili uendelee, tunafanya mambo hayo kama yameundwa ama la. Kama unayo Kweli, basi dumu na Kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini acha iwe ni Kweli ya Biblia kwanza! Angalieni, kwa ninii . . . wakati huu wa Laodikia.

144 Nao manabii, ah, Roho Mtakatifu akizungumza kupitia kwa Paulo, ambaye alikuwa ni Masihi. Haikuwa ni Paulo, ilikuwa ni Kristo! "Mungu, katika zama za kale na kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu kwa njia ya manabii, katika siku hizi za mwisho kwa Yesu Kristo," Waebrania 1, tazameni, Roho Mtakatifu, Kristo, Injili iliyowekwa msingi katika Kristo, Neno lililowekwa msingi katika Kristo. Na kama imewekwa msingi katika Kristo, na imethibiti- . . . Mungu ataithibitisha kwamba ni Kweli.

145 Hiyo ndiyo sababu ninyi Wapentekoste mnampokea Roho Mtakatifu katika imani ya Methodi- . . . mbele ya utakaso wa Methodisti, kwa sababu mlikuwa kwenye Neno hasa.

146 Hiyo ndiyo sababu ninyi Methodisti mlitakaswa wakati Walutheri hawakuuamini, mlikuwa kwenye Neno.

147 Hivyo ndivyo ninyi Walutheri mlivyopata kuokoka, mkahesabiwa haki, kwa sababu mjumbe wenu alihubiri kuhesabiwa haki, na akalipinga kanisa Katoliki ambalo lilikuwa limeenda kombo sana kuliko yote. Waliamini kanisa tu; mlirejea kwenye Biblia, nanyi mkachukua kweli hiyo ya Biblia na kuishikilia.

148 Ndipo basi moja kwa moja akaja Wesley akiwa na kweli nyingine, naye akaishikilia; moja kwa moja ikaja Pentekoste pamoja na kweli nyingine, na kuishikilia; basi kama mnaweza kuushikilia huo na kuona ni kweli, mbona basi msichukue kitu hicho chote ambacho kimethibitishwa kuwa ni kweli? Liamini lote!

149 Sasa, wakati tunapowaona wajumbe hawa, tunajua basi. Tunamwona Kristo, yule Mungu-Nabii mkuu akiyabashiri

mambo haya kutukia katika siku za mwisho. Inafanya nini? Inautambulisha wakati wa mazao. Inautambulisha wakati ambao mazao yatavunwa, yale yatakayokuwapo katika siku za mwisho. Mnaliona?

150 Sasa, mambo haya yatakuwa katika siku za mwisho. Tunajua tunatarajia zao la aina gani. Tunatazamia kanisa ambalo wakati mmoja lilikuwa na Nuru, likaiondokea, likaenda kwenye madoido ya ulimwengu, yote yakapigwa msasa (hiyo ni kweli?), wanaondoka, wakiingiza kila namna ya mfuasi, na chochote kile, na kukiita Wapentekoste, wanabatiza kitu chochote.

151 Maji hayamwokoi mtu. Inahitaji Damu ya Yesu Kristo. Hakuna uhai katika maji. Uhai huja katika seli ya Damu; inahitaji utakaso kusafisha maisha hayo, kuangamiza tamaa ya dhambi; ndipo Roho Mtakatifu anaingia kwenye vyombo hivyo safi na kuviweka kando katika kazi, utumishi. Madhabahu yalikitakasa chombo, bali ninii. . .kujazwa kwake ndiko kulikokiweka katika utumishi. Kiliwekwa kando *kwa ajili ya* utumishi, sasa hakina budi kuwekwa katika utumishi. Naye Roho Mtakatifu huliweka kanisa katika utumishi. Nilikuwa ninaupenda ule wimbo mdogo:

> Walikuwa wamekusanyika kwenye chumba
> cha juu,
> Wote wakiomba katika Jina Lake,
> Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
> Nazo nguvu za utumishi zikaja.

Naam. Na hicho kingine kinasema:

> Aliyowafanyia siku hiyo
> Anaweza kuwafanyia vivyo hivyo. (Hakika.)

152 Lile zao; manabii; tulisimama hapo juu ya Kristo. Sasa turudi tu nyuma kidogo.

153 Isaya, nabii, jinsi alivyoshuhudia, akatabiri juu ya wakati wa mwisho. Yeye alisema, "Mwili wote ungekuwa vidonda vilivyojaa usaha, kila meza itajaa matapiko!" Mbona, wanaume na wanawake leo hii, wanakula ushirika, huku wanaishi na wake wawili au watatu, ama waume wawili au watatu, (kweli) kila namna ya. . .wakivuta sigara, na mambo hayo yote; wakija kanisani, wakila ushirika!

154 Sasa, ningeshuka kidogo tu kuliko hapo, bali nitangojea tu kidogo, labda si vizuri basi. Nilijisikia kuzuiwa kidogo juu ya yale niliyokuwa nikitaka kusema. Lakini mimi. . .Unaweza kusoma katikati ya mistari. Mnajua yale Biblia inayosema, kwamba mambo ya kawaida na yasiyo ya kawaida ni yapi.

155 Mambo haya yote tunayoona yakitendeka basi, na taifa. . . sayansi inasema ni. . .miaka minne ama mitano iliyopita, "Ni dakika tatu ifike usiku wa manane." Israeli wako kwenye nchi

ya uenyeji wao. Kanisa liko katika Laodikia. Loo, jamani! Tunatafuta nini? Kuna shida gani?

156 Tunaitafuta Nuru ya jioni. Loo, nashangaa, kama ingekuja, kama tungeitambua? Ama ingeruka juu ya vichwa vyetu kama ilivyofanya huko nyuma katika nyakati zingine? Kamwe hawaijui mpaka imekwenda mbali kupita kiasi.

157 Mnakumbuka, hao watu wa kidini ndio waliowaua manabii waliotumwa kwao. Yesu alisema hivyo. Yeye alisema, "Enyi wanafiki!" Kasema, "Mnayapaka chokaa makaburi ya manabii, nao baba zenu ndio waliowaweka mle ndani kisha mnayajenga makaburi yao."

158 Hebu liangalieni kanisa Katoliki ya Kirumi, lililipaka chokaa kaburi la Mtakatifu Patrick, likalipaka chokaa kaburi la—la Joan wa Arc. Walimwua mwanamke huyo, na kumchoma moto kama mchawi, kwa sababu alikuwa ni wa kiroho, kwa sababu aliona maono. Walimchoma moto kwenye nguzo, kama mchawi. Miaka mia mbili baadaye wakaifukua miili ya hao makasisi na kuitupa mtoni, kufanya vitubio, wakijua ya kwamba alikuwa ni mtumishi wa Kristo. Lakini, katika siku hiyo, wao hawakujua yeye alikuwa ni nani, wakati kanisa lilipokuwa likipita.

159 Nalo litaenda moja kwa moja juu ya vichwa vya watu nao hawatalitambua.

160 Yesu, hao hawakujua kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu mpaka alipokuwa amekufa na kuzikwa na kufufuka tena. Hivi Petro hakuwashtaki kwenye Siku ya Pentekoste? "Ninyi watu kwa mikono mikatili mmemsulibisha Mfalme wa Uzima, na mkauua, mkamwua!"

161 Loo, kimulimuli chekundu cha ishara ya kuja Kwake kimeinamishwa! Amina! Tuko mwisho. Amina. Ishara hiyo ya kimulimuli chekundu iko kila mahali, kila mahali, "Ikabodi," imeandika juu yake. Wakati umekwisha. Wakati umekwisha!

162 Sayansi imefikia mwisho wao. Hiyo ni kweli. Wamevumbua kitu fulani sasa hata wanaweza kuulipua ulimwengu mzima, kila mtu anamwogopa mwenziwe. Wako kwenye wakati wa mwisho.

163 Ustaarabu, umefikia mahali watu . . . ule mnara unabembea kinyumenyume. Watu hawatendi kama watu wastaarabu. Ungeweza kuwazia mtu akitaka kuwa mhuni, huku masharubu yake yananing'inia chini namna *hii*, mikanda yake ikining'inia kutoka kwenye nyonga zake, akishuka kupitia kwenye uwanja wa shule namna hiyo? Akili ya ulimwengu ujao baada ya huu, iwapo kuna ya zaidi, kutoka na wasichana wadogo wa miaka kumi na minne, hao huko nje mtaani.

164 Leo hii, katika moteli yangu, mama mmoja alilala huko nje asiyekuwa na nguo za kutosha kujikinga na bunduki ya gobori, naye mumewe amelala huko nje vivyo hivyo, na huo upepo

baridi. Wanafikiri mwili wao ni wa kuvutia sana inawabidi kuuonyesha. Hivi hamtambui huyo ni ibilisi? Hiyo ni kweli. Wakivua nguo zao, ni wendawazimu tu wanaofanya hivyo. Legioni alifanya hivyo kwa sababu alikuwa mwendawazimu. Tazama! Nasi tunalo hilo, bali hilo linaitwa "mtindo," unaoitwa "wa kisasa." Tunauita "Ibilisi!" Ninayo Biblia kuthibitisha ya kwamba ni ibilisi. Ni kupagawa na ibilisi, kupagawa na pepo (sio kuteswa). Kupagawa, yeye amekupata! Hiyo ni kweli. Ati uwaambie juu yake? Watalipuka. Hawataki uhusiano wowote na Hilo! La, bwana. Wanayo mawazo yao wenyewe, kwa sababu kwenye nyumba yao ya kuhifadhia maiti wanayohudhuria kamwe hawakemei hilo. Kuvutia kijinsia kunafanywa shuleni na makanisani, nao wachungaji wanaogopa kukukemea, kwa nadra sana watasema chochote.

165 Nilimsikia mhudumu mmoja hivi majuzi, alisema, "Hapo walipovumbua kitu hiki cha samawati kwa ajili ya macho, na—na midomo myekundu, waliufanya ulimwengu wa kupendeza zaidi." Mhudumu wa Injili, mimbarani, angetoa tamshi la namna hiyo, anahitaji safari ya kwenda Kalvari. Kweli. Hiyo ni kweli kabisa, wakati Biblia inalihukumu!

166 Nalo kundi la Kipentekoste lilimwambia dada fulani ambaye (alikuja mahali pale, akilia) kwa sababu alikuwa amezisokota nywele zake nyuma ya kichwa chake, akiwa na nywele ndefu, kasema, "Huenda tairi yako ya akiba ikatoka pumzi." Kasema, "Huna budi kuzikata nywele hizo, kwa sababu Biblia ilisema alikuwa . . . katika Isaya, mlango wa 5, alikuwa na tairi duara kama mwezi." Sasa, Biblia inawezaje kusema ya kwamba "mwanamke anayefanya kitu kisicho cha kawaida," hastahili kuishi naye anapokata nywele zake, anathibitisha ya kwamba anaaibisha kichwa chake, halafu nywele ndefu . . . ? . . . Unawezaje kuifanya Biblia kusema jambo kama hilo? Vema, wanawake wetu wa Kipentekoste wana shida gani? Mmeona televisheni kupita kiasi! Mmeona ulimwengu mwingi kupita kiasi, wala Neno la Mungu la kutosha haliwavutii. Sasa, Biblia ilisema hivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo si mimi, sasa, hiyo ni Biblia!

167 Loo, kuvutia kijinsia! Mama mmoja aliniambia sio muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiendelea kuhusu wao kuvaa hizi kaptura, kasema, "Mimi—mimi huvaa suruali ndefu."

168 Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi." Ninyi . . . Biblia ilisema hivyo. Hawezi kubadilika.

169 Unasema, "Hao ni Baptisti." Hao ni Wapentekoste. Ninazungumza *nanyi*. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

170 Lakini kuna shida gani? Kuna shida gani? Mtu fulani alilegeza kamba mahali fulani. Maskini mzee mhubiri rafiki yangu alizoea kusema:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
Tukapatana na dhambi;
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka,
Lakini mbuzi waliingiaje?

171 Kuna shida gani? Mnapolegeza kamba, kamba za Neno la Mungu! Kumbukeni, ulikuwa ni mpango wa Mungu kulizingira Kanisa Lake kwa Neno Lake, hapo mwanzo.

172 Ndipo wakati Hawa alipotoa hoja na kusema, "Vema, sasa, si ni jambo la maana, ningeweza kuishi vizuri tu kama wao . . .?" Aa! Hilo lilitosha.

173 Na hilo daima limetosha. Hiyo ndiyo sababu yeye alikatazwa kuwa mhubiri. Mnaona, ililegeza tu kamba. Hapo ndipo (kanisa) misingi yake ilipoanguliwa, katika Pentekoste, na huo ndio msingi. Hakuna Maandiko kwa ajili yake. Mnaona? Sasa, unafanya nini basi? Unapata mkusanyiko ule ule uliopata kule nyuma katika Edeni. Angalia, sasa, ndipo tunapokuja kwenye Neno, mnasema kulihusu Hilo . . .

174 Hakuna mtu anayeweza kustahimili Hilo! Ninampa changamoto mtu yeyote kusema hilo. Nilihubiri juu ya *Uzao wa Nyoka*, wengi sana wakalipuka juu yake. Nimewaomba baadhi ya watu waje wanikabili juu yake. Siwapati.

175 Huko Chicago sio muda mrefu uliopita, mnazo hizo kanda, walidhani walikuwa wamenitia mtegoni katika jambo fulani. Walikuwa na Shirika lote Kuu la Wahudumu wa Chicago, Ndugu (Anaitwaje?) Tommy Hicks, Ndugu Carlson alikuwako. Basi siku mbili usiku kabla ya hapo, Bwana aliniamsha usiku, kasema, "Nenda ukasimame pale dirishani." Nikaenda, na kulikuwa na dhoruba. Akasema, "Sasa, wamekuwekea mtego." Akasema, "Kwenye kiamshakinywa hiki, usiogope. Endelea, nitakuwa pamoja nawe." Sasa, hili ni katika Jina la Bwana. Mnaweza kuwauliza mpate kujua. Liko kwenye kanda, lilitabiriwa hapo kabla: Kasema, "Sasa, usiogope kwenda, bali nenda ukasimame," kasema, "Nitakuwa pamoja nawe."

176 Basi kesho yake nikakutana na Ndugu Carlson, kiongozi wa lile tawi kule, na Tommy Hicks. Naye akaniambia ningekutana nao kisha twende mahali palipoitwa "Town and Country" kwa ajili ya kiamshakinywa. Nikaketi pale chini vivyo hivyo hasa. Nikasema, "Ndugu Hicks, wewe ni daktari wa uungu nasi tunaenda kukutana na kundi kubwa la wahudumu hapa, shirika lao la Chicago, mbona usiende ukazungumze kwa niaba yangu? Nimekufanyia mambo mengi sana." Nilikuwa tu nikimjaribu.

Akasema, "Loo, nisingeweza kufanya hivyo, Ndugu Branham."

177 Nikasema, "Vema, kwa nini usiendelee?" Nikasema, "Mimi ningekufanyia lolote, sasa mbona usinifanyie tu hilo?"

178 Akasema, “Loo, nisingeweza kufanya hivyo, Ndugu Branham. Wasingevumilia hilo.”

Ndugu Carlson akasema, “La, wasingelivumilia.”

179 Nikasema, “Mnajua ni kwa nini.” Nikasema, “Hebu niwaambie jambo fulani, ni kwa sababu ninyi, nyote wawili, mnajua kwamba wamenitegea mtego wa swali.” Ndipo nikasema, “Mnao.” Sasa, hili liko kwenye kanda. Kama mkitaka kanda hiyo, tunaweza kuwa nayo. Nanyi mnawafahamu watu hawa wote. Kwa hiyo nikasema, “Usiku uliotangulia jana, niliona ono kwamba tungeketi hapa asubuhi ya leo na Tommy angelikataa hili.” Nikasema, “Sasa angalieni, ninyi ni . . . mmekikodisha chumba kile cha hoteli.”

“Naam.”

“Mmekilipia.”

“Naam,” Ndugu Carlson.

180 “Bali hamtakihifadhi. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI!”

“Kwa nini?”

181 “Mtaenda mahali pengine. Hicho ni—hicho ni chumba cha kijani; tunaenda kwenye chumba cha hudhurungi. Nitakuwa pembeni; Daktari Mead ataketi mkono wangu wa kulia; na yule mzee mhudumu mweusi pamoja na mke wake wataketi huku kushoto,” jinsi hasa itakavyokuwa. Kisha nikasema, “Ninyi angalieni sasa, njoni tu moja kwa moja. Mmemwona Mungu akiwaponya wagonjwa, mwangalieni katika vita wakati mmoja!” Nikasema, “Yeye ni mkuu, wa ajabu sana.” Nikasema, “Angalieni tu hayo maswali muone jinsi kutakavyokuwa kimya.”

Basi tulipofika pale asubuhi hiyo . . .

182 Kama mkitaka hiyo kanda . . . Jim, unayo, hujaileta? Papa hapa, papa hapa, mnaweza kuwa na hiyo kanda mkiitaka, kwenye mkutano.

183 Nikasema, “Mna kitu gani dhidi yangu? Mna shida gani nyinyi jamani?”

184 Ndugu Carlson akasema, “Vema, Ndugu Branham aliniambia siku mbili zilizopita ya kwamba ingetubidi . . . ” Wala hawakulipata jengo hilo, walilibatilisha. Wasingewaruhusu kulichukua kwa sababu kundi la muziki lililichukua nao hawakujua walikuwa wametoa malipo ya kwanza kwake, basi iliwabidi kulibatilisha kwa Wafanyabiashara. Na labda mliusikia ujumbe wake, Ndugu Williams hapa, na hapa, pia. Na—na—naye alisema, “Ndugu Branham aliniambia mahali hasa kila mtu atakapoketi, na kuniambia kile hasa kingetukia.” Kasema, “Jambo moja,” kasema, “Mimi . . . wengi wetu huenda wasikubaliane na Ndugu Branham juu ya Ujumbe wake, lakini,” kasema, “itatubidi kukubali jambo moja, yeye haogopi

kuutangaza," kwa hiyo—kwa hiyo basi akasema, "hana woga na Huo." Kasema, "Sasa, haya basi, Ndugu Branham."

185 Nikasema, "Sasa, kabla hatujaanza, ninataka mtu fulani, juu ya jambo fulani ambalo nimesema, aichukue Biblia hiyo na kusimama hapa karibu nami." Basi hilo lilikuwa ndilo kundi nyamavu kuliko yote nililopata kulisikia. Nikasema, "Basi, kama hamwezi kuliunga mkono, basi ondokeni mgongoni mwangu! Naam. Ndugu, niko hapa kuweka mabega yangu pamoja na yenu, lakini inatubidi kurudi kwenye kanuni za Biblia."

186 Kasema, "Kwa nini—kwa nini usiwaache hao wanawake? Loo, naam, wewe ni . . . watu wanakuamini wewe kuwa ni mwo—mwonaji wa Mungu."

Nikasema, "Sikusema hayo kamwe."

187 Akasema, "Lakini watu wanaamini hilo." Kasema, "Kwa nini—kwa nini usiachane na hao wanawake?" Kasema, "Na uache kuwaambia jinsi ambavyo wanapaswa kuvaa nguo na kukata nywele zao na vitu wanavyopaswa kutumia. Kwa nini usiachane nao? Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupokea karama na—na kufanya jambo fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu?"

188 Nikasema, "Ninawezaje kamwe kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?" Hiyo ni kweli. Inawabidi kurudi kwenye msingi wa mwanzoni.

Mungu, uturehemu sasa. Naam, bwana.

189 Sisi hapa, wakati wa mwisho! Taa nyekundu imeinamia, inamulika! Kuja kwa Bwana kumekaribia. Naam, bwana. Sikilizeni! Ujumbe wa wakati wa mwisho unapaswa kutimiza masharti ya wakati wa mwisho. Mahali walipoenda kombo, Ujumbe unapaswa kuwarejesha. Sikuzote, Ujumbe wa wakati wa mwisho hutimiza masharti ya wakati wa mwisho. Kote katika Maandiko. Itabidi ufanye hivyo wakati huu, wito wa kurudi kwenye Neno la asili. Loo, jamani! Kama wajumbe wengine walivyofanya siku hizo, Ujumbe huu itabidi uwe vivyo hivyo. Tumeahidiwa hilo! Mungu aliliahidi katika Neno Lake! Malaki 4, ilisema itatukia, "Na kuirudisha Imani ya watoto iwarudie baba zao." Iliahidi hilo, nasi tunaishi katika siku hiyo!

190 Loo, imekuwa hivyo daima, kila wakati, kundi la viongozi linalowafanya watu wachanganyikiwe kabisa. Sana sana sio hao watu; ni viongozi ndio wanaowafanya wachanganyikiwe. Sasa hebu . . .

Mnasema, "Loo, Ndugu Branham!"

191 Vema, sasa, hebu kidogo tu sasa, hatuna budi kulifanya hili la Kimaandiko. Kama si Maandiko, basi halifai kitu. Kwa maneno yao ya hekima, katika uongozi wao usio na uvuvio, maneno ya hekima ya kilimwengu, wao . . . Mbona, kuna baadhi ya hao wenye vipaji wanaoweza kuyaweka hayo

pamoja, bali mnafikiri Shetani hana kipaji, pia? Hivi yeye, vema, hakumkaribia Yesu Kristo na kumpa sababu, na hata akamnukulia Maandiko? Alifanya hivyo! Yeye ni bingwa wa hilo. Lakini Yesu kamwe hakubishana naye, Yeye alisema, "Imeandikwa, pia! Rudi nyuma Yangu, Shetani." Naam, uongozi usio na uvuvio.

192 Mwangalieni Kora, katika siku ambazo Mungu alimtuma Musa na ujumbe, naye Kora na Dathani wakawazia, wakamwendea Musa, na kusema, "Sasa, hebu kidogo, unajichukulia mengi kupita kiasi! Unafikiri wewe ndiwe changarawe ya pekee ufukoni; bata kidimbwini, ndiwe wa pekee. Nitakufahamisha wapo watu wengine walio watakatifu, pia!" Musa hakusema hawakuwa watakatifu. Lakini yeye alikuwa na agizo, ilimbidi kulitekeleza. Ndipo wakaunda kundi na walikuwa wakija kumpinga Musa.

193 Basi Mungu akamwambia, "Nendeni mkasimame pale mlangoni." Watu hao walikuwa na chetezo mkononi mwao, nanyi mnajua kile hicho chetezo kingalifanya. Mungu aliifungua ardhi ikawameza. Nao walikuwa na moto kutoka madhabahuni, ndani yake. Wakiwa na moto katika chetezo, wa kimsingi kama ilivyokuwa, walishindwa kuutambua huo ujumbe.

194 Mungu akasema, "Ninakutuma, Musa, huko chini kufanya hivi. Wewe walete hapa."

195 Mnaona, walishindwa kuliona. Musa alikuwa "mnyofu" sana kwao. Kama vile Eliya alivyokuwa, kwa ile Shule ya Manabii, "mnyofu kupita kiasi," alidumu na Neno.

196 Hivyo ndivyo ninyi Wapentekoste, iliwabidi kujitenga na ulimwengu wote, mkae sawa na Neno. Sasa msififie mrudi kwenye kitu kile kile mlichotoka kwake, mnateleza! Msiitenganishe nanga yenu kutoka Kalvari. Lishikilieni Neno la Mungu, kwa kuwa "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu," dumuni na Hilo.

197 Sasa, Dathani na hao walidhani walikuwa . . . kungekuwako na watu wengine. Mnaona, hiyo ni akili ya kibinadamu ikijaribu kuingiza mawazo yao kwenye mpango wa Mungu. Hilo ni zuri. Akili ya kibinadamu ikijaribu kuingiza mawazo yao katika Neno la Mungu. Haitafaulu! Haitafaulu. Kamwe haijawahi kufanya kazi wala haitafanya kazi.

198 Mwangalie Yesu wakati Yeye alipokuwa amesimama pale, kasema, "Ni yupi kati yenu anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Ni nani kati yenu anayeweza kuonyesha ya kwamba sijafanya yale hasa Maandiko yalisema Mimi nitafanya? Ninadai kuwa Masihi. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msininii, msiniamini Mimi. Lakini kama nikizitenda zile kazi wala hamwezi kuniamini, aminini kazi nizifanyazo, zinanishuhudia Mimi." Kweli kabisa. Nao wasingeweza kuamini, walitaka njia zao wenyewe.

199 Huenda wasimaanishe kufanya hivi na wakosee. Hawamaanishi . . . Siamini mtu anamaanisha kufanya hivyo. Ninawaona watu wengi wazuri huko nje kwenye makanisa hayo makubwa ya kimadhehebu. Ninawaona watu wazuri. Lakini ni kama vile yule mwanasheria alivyosema kwenye redio, nikishuka kuja huku, "Jambo la kushangaza, ni kwamba jinsi ambavyo makasisi wangeweza kusimama mimbarani, na kuona nyakati hizi zikija, wala hasira yao ya haki isichochewe, juu ya dhambi za ulimwengu!" Basi wakati inapombidi mwanasheria kusimama na kusema hivyo! "Na jinsi ambavyo walei wangeweza kutumia fedha zao kwa kila namna ya bustani za wanyama pori na mbuga za wanyama, na kadhalika, wala wasidhamini mpango wa wamishenari, kuupelekea ulimwengu Injili."

200 Wakati wamishenari wenye njaa, wasio na viatu miguuni mwao . . . Haleluya. Hakuna dhehebu la kuwaunga mkono, kwa sababu, msimamo wao kwa ajili ya Neno la Mungu. Hakuna kitu cha kuwaunga mkono. Ukiwapata wakiwa na kitu cha kuwaunga mkono huko nje, basi wana kitu gani? Lundo kubwa la mafundisho ya sharti. Mmishenari halisi, wa kweli, na ishara zikimfuata, inambidi kutegemea mwanamke fulani mfua nguo kujihifadhia mapeni machache. Tazameni, haya basi.

201 Huenda wasimaanishe kufanya . . . Vema, bali wana shida gani? Wao ni vipofu. Yesu alisema hivyo. Kumbukeni, kumbukeni, Yesu alisema jambo lile lile. Na inaonekana kama, siku hizi . . .

202 Sasa sikilizeni, ninatumaini mimi sikosoi. Wakati unapoufanya ukweli usi—usijisikie ninakosoa. Ninajaribu tu kuninii . . . Na—napenda . . . Na ikiwa huninii . . . Nina—nina bidii ya Kanisa. Hili, wao labda ni kanisa la Assembly of God, ama chochote lilicho, ama—ama si—sijui ni kitu gani. Nini . . . Haileti tofauti yoyote kwangu. Ni kanisa la Mungu. Hivyo ndivyo lilivyo, ninaamini, ni kanisa la Mungu. Vema, sasa, sote tunapaswa kuwa hivyo, sio kanisa la kimadhehebu la Mungu, bali inatupasa kuwa Wakristo moyoni. Kanisa la Mungu linaishi ndani ya kuta, sio jina, kadhalika.

203 Sasa, leo hii limezidi sana katika hili, kwamba uanachama ndio tu unaojalisha kwa watu. Sasa, iangalieni Baptisti ikiwa na uamsho. Loo, wamekuwa na mmoja. Walikuwa na msemo katika mwaka wa '44, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Ujumbe wa Billy Graham ukiendelea. Mbona, hakika, umefanya jambo kubwa. Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, imekuwa ni jambo kubwa, bali tumepata nini?

204 Yesu aliwaambia Mafarisayo, "Enyi viongozi vipofu wa vipofu. Mnazunguka bahari kufanya mwongofu mmoja, naye ni mara mbili mwana wa kuzimu kuliko alivyokuwa alipoanza." Na hao ndio tulio nao siku hizi.

205 Billy Graham, nilipohudhuria kiamshakinywa chake huko Louisville, Kentucky, alipanda pale, akiwa mwinjilisti mkali alivyokuwa, akasema, "Ninaenda . . . Paulo alisema . . . Huu hapa mfano." Kasema, "Paulo aliingia mjini na kumpata mwongofu mmoja, akarudi mwaka mmoja baadaye naye alikuwa na thelathini kutoka kwa huyo mmoja." Kasema, "Mimi huenda mjini na kupata waongofu elfu thelathini, kisha narudi katika mwaka mmoja na siwezi kupata thelathini." Akasema, "Kuna nini?" Nami nilipendezwa na mtazamo wa huyo mwinjilisti. Akaelekeza kidole chake huko nje, yapata watu mia tatu wameketi pale, akasema, "Ni ninyi kundi la wahubiri wazembe." Akasema, "Mnaketi ofisini huku miguu yenu ikiwa juu ya dawati, kisha mnampigia mtu simu, na kumwomba ashuke aje na—na kujiunga na kanisa lenu. Mnapaswa kwenda kumtembelea."

206 Niliketi pale, nikawazia, "(Ee Mungu!) Unajua, Mwinjilisti Billy, wewe ni mtu mashuhuri. Mimi ni—mimi ni mpumbavu. Lakini hebu nikuulize jambo fulani." Laiti ningaliweza kugeuka na kusema hivi; lakini na—na—navutiwa na huyo ndugu, nafikiri ni mtumishi wa Mungu. Lakini ningalipenda tu kusema hivi, "Basi, Billy, ni mhubiri wa aina gani Paulo aliyekuwa naye wa kumfuata huyu?" Ni kitu gani kilichotukia? Paulo hakumwacha tu ainue mkono wake afanye maamuzi, alimpeleka hadi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, akaiwasha moto nafsi yake, wala asingeweza kutulia.

207 Hiyo ndiyo shida ya siku hizi, ni uanachama. Naam. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . washiriki, uanachama mkubwa, madarasa makubwa ya shule ya Jumapili, kumpa mtu zawadi ambaye anaweza kuongoa na kumleta mtu fulani kutoka kwa kanisa lingine humu, ni nani aliye na wengi zaidi. Mwajua, huo ni Ufarisayo! Kisha kujivunia hilo sana, "Tuliwashinda Jumapili iliyopita." Kama mmefikia mahali ambapo inawabidi kulifanya kanisa la Mungu mashindano ya hadhi, basi huo ndio wakati wa kufunga milango mwende nyumbani.

208 Kanisa la Mungu ni chombo kilicho hai cha Mungu duniani, likimdhihirisha Yesu Kristo. Ninajua Hilo halipendwi sana na watu, huwezi kutarajia lipendwe. Tunatarajia kuwa sahihi.

209 Wanafanya majivuno makubwa juu yake . . . Lakini, hivi ulijua, zile kelele kubwa hazikumwathiri nabii Eliya. Yeye aliusikia moto na moshi ukipita, na ngurumo na radi, na damu na mafuta, na kila kitu kingine, havikumsumbua. Mwajua, Marekani daima inatazamia jambo fulani kubwa lililo na kelele nyingi ndani yake. Bali Mungu ni "Sauti ndogo tulivu" inayomvutia nabii.

210 Mwajua, mkokoteni siku moja ulienda nje shambani, nao unagongagonga, ukifanya kelele nyingi sana wakati ukienda huko shambani. Na wakati ukirudi, ulipitia kwenye matuta yale

yale wala haukufanya kelele hata kidogo, ulikuwa umejaa vitu vizuri. Mnaona? Naam.

211 Lakini tunaweka ujuzi wetu juu ya lundo la makelele. Tunawezaje kufanya hilo? Tunawezaje kufanya mambo hayo jinsi hiyo? Loo, jamani! Kisha kuyabandika madoido ya Hollywood ndani, kuwaleta wanawake mimbarani, wamevaa nguo zilizowabana sana na kuonekana wazinifu, wakicheza katika roho. Sijui ni roho ya namna gani!

212 Simaanishi kuwa mkosoaji sasa, ni—nina—nina . . . ni—ninawapenda. Kama siwapendi, basi Mungu atanihukumu endapo nina kusudi lolote lingine mbali na hilo. Mnaona?

213 Lakini mnalipata hilo, mnaona. Huko ndiko Wapentekoste walikoelekea. "Tuna zaidi ya yale yule ndugu pembeni aliyokuwa nayo." Loo! "Tuna mengi kuliko Assemblies, kwa kuwa sisi ni wa Umoja, ama sisi ni wa Utatu, na sisi ni . . . " loo, *hili, lile,* ama *linginelo,* chapa zo—zote mbalimbali walizo nazo, mnaona. Loo, ndugu, hilo halimaanishi *hicho* kwa Mungu. Yeye hushughulika na mtu binafsi. Kweli.

214 Angalia, kelele nyingi, bali hazikumvutia nabii. Huyo nabii hakujali kuhusu hizo kelele nyingi. Lakini alipoisikia ile Sauti ndogo tulivu, alijua ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno, akaufunika uso wake akatoka nje.

215 Mwajua, jua linaweza kuvuta maji mengi zaidi katika dakika kumi na tano, pasipo na kelele yoyote, na sisi . . . zaidi ni kel- . . . nasi tunapiga kelele nyingi zaidi tukichota galoni ya maji kuliko jua lifanyavyo kwa galoni milioni moja. Hiyo ni kweli. Daima tunatafuta kitu kilicho na "shangwe" kubwa na tele, na shamrashamra nyingi ndani yake. Na inapofikia kwenye kanuni ya kulichukua Neno, ndipo hiki hapa hicho kitu kinainuka. Mnaona? Kinakuja, nao wanasema, "Vema, Mungu abarikiwe, nakwambia . . . "

216 Nilikutana na mtu hapa sio muda mrefu uliopita . . . Sisemi hili ili kukufuru, samahani tafadhali ikiwa mimi . . . mawazo yangu yanalifanya la kukufuru. Nilikuwa kwenye mkutano wa hema na, yule mhudumu, mhudumu wa Kipentekoste akamleta mke wake huko kupiga piano. Basi aliponitambulisha kwa mkewe, kwa kweli, karibu nizimie. Huyo mwanamke alikuwa na nywele fupi kwelikweli, zimetiwa mawimbi, naye alikuwa na herini kubwa, nene, na rangi ya kutosha midomoni mwake, ama vyovyote kitu hicho kilivyo, makucha ya vidole yamepakwa rangi. Alionekana kana kwamba alikuwa ni . . . Ilionekana ya kuchukiza sana; makucha makubwa mno, marefu, na jinsi hiyo. Na amevaa nguo zilizoonekana za kizinifu; ndogo, zilizobana, fupi, hata asingeweza kuziweka juu ya magoti yake alipoketi. Vema, nilisimama hapo kidogo, nami nikasema, "Ndugu, hivi nitadhuru hisia zako kama nikisema jambo fulani?"

217 Akasema, "Mbona, bila shaka hapana." Mtu mzuri, naye huyu alionekana ni mwanamke mzuri.

Nikasema, "Hivi unasema mke wako ni mtakatifu?"

Kasema, "Naam."

218 Nikasema, "Kunradhi hili tamshi, bali anaonekana kama 'mtakataka' kwangu mimi," Nikasema, wajua, "ama kitu kama hicho." Nikasema . . .

219 Akasema, "Unamaanisha nini, Ndugu Branham?" "Loo," akasema, "wewe ni wa mrengo wa zamani."

220 Nikasema, "Mimi ni wa mrengo wa Maandiko. Hiyo ni kweli, mrengo wa Maandiko." Siamini ya kwamba mtakatifu hufanya hivyo, siwezi kabisa kuamini, wakati Biblia inalihukumu. Unaona?

221 Vema, inaonekana, kila wakati, kila kitu tunachosikia, "walikuwa na ukata shauri arobaini," "ukata shauri arobaini na nne," "tulikuwa na ukata shauri mia tatu." Vema, hilo ni ungamo. *Maungamo* ni "mawe." Hiyo ni kweli, maana Petro, juu ya ungamo lake, aliitwa "jiwe, jiwe dogo." Petro, ungamo lake. Sasa, mawe ni sawa, lakini yanafaa nini ama jiwe lina faida gani kwa jengo kama hakuna mwashi halisi mwenye kifaa kikali cha Neno kuyakata na kuyafanya wana wa Mungu? Mnaona? Ungamo lina faida gani?

222 Hiyo ndiyo sababu unarudi wala huwezi kupata thelathini kutoka kwa elfu thelathini. Unayabingirisha tu mawe kutoka mavumbini, na kuyabingirisha huko nje, nayo hayafai kwa ajili ya hekalu bado. Hayana budi kukatwa, kupimwa kwa Neno la Mungu, kuwekwa mle ndani, yakaunganishwa pamoja, kujengwa juu ya msingi wa Fundisho la mitume, Yesu Kristo jiwe la Pembeni. Naye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hiyo ni kweli.

223 Tunawezaje kuwa Kanisa wakati tunadharauliana? Yeye alisema, "Hivi watu wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Tunapobadilisha dini na kuvunjika, na kwa ajili ya tofauti ya kimadhehebu . . . Siwalaumu hao watu, ninalilaumu dhehebu. Hiyo ni kweli. Sio watu hata kidogo. Mnaona? Loo, ni vibaya sana, hata hivyo mimi . . .

224 Inakubidi kuwa na kifaa hiki kikali, Neno la Mungu, kuwachonga wawe wana wa hilo Jengo. Loo, jamani! Ombi langu ni, "Mungu, fanya hima na Malaki 4. Tupe ujumbe katika siku za mwisho. Tupe mtu fulani, tuma kitu fulani cha kuliokoa kanisa hili la Kipentekoste."

225 Mungu angetuma mjumbe wa namna gani kwetu kwa ajili ya siku hizi za mwisho? Nitakwambia hivi, ndugu yangu, dada, kama ndugu yako na mtumishi mwenzako anayeutazamia wakati huo kuja, yeye atakuwa ni mjumbe wa namna ile

ile kama aliyekuja kwa wakati ule mwingine. Namna ile ile! Angelirudisha kanisa kwenye Neno. Mungu, jalia tuweke msingi kwa ajili yake kabla halijafika hapa. Kabla hajaja, jalia tuweke msingi na tuwe mawe, yaliyokatwa, tayari kusimama bega kwa bega pamoja naye wakati Mungu atakapomtuma, kwa sababu Yeye aliahidi ya kwamba atalitenda.

226 Sasa, ninajua, ninahisi hilo likirudi. Na, kumbukeni, kwa karama ndogo ninaweza kushika utambuzi wa roho, mnaona. Sasa, mnachukia hilo, niliposema Malaki 4. Lakini hebu niwaambieni jambo fulani. Mlisema, "Yesu alisema, 'Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye Eliya aliyenenwa habari zake.'"

227 Lakini kama mkiona yale Yeye aliyosema katika—katika—katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 11 na kifungu cha 6, "Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa, na kusema, 'Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.'" Hiyo ilikuwa ni Malaki 3, sio Malaki 4.

228 Kwa kuwa, katika Malaki 4, Yeye alisema, "Kabla siku hii haijaja, dunia ingeteketezwa nao watu wengetembea juu yake; itateketezwa kama makapi." Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa akinena basi juu ya yule mjumbe mbele ya uso Wake, ambaye alikuwa Eliya, hilo linasema . . .

229 Si—siamini katika upuuzi huu wote unaoenea kote leo juu ya joho la Eliya na upuuzi huo wote. Mimi . . . Mabandia hao wote hawana budi kuja, hakika, kuvuruga kitu kilicho halisi kitakapokuja. Lakini, hebu niwaambie, atainuka mjumbe mwishoni mwa wakati huu wa Kipentekoste naye atalimalizia hili jambo. Itakuwa ni mtu. Sio kundi, si dhehebu; bali mtu mmoja. Daima imekuwa hivyo, wala Mungu hawezi kubadilisha ratiba Yake, Yeye ni Mungu wa Milele.

230 Kumbukeni, kama mjumbe huyo (Yohana) alikuwa ndiye mjumbe wa Malaki 4, basi Maandiko yalikosea, kwa kuwa yalisema, "Ingeninii . . . dunia itateketezwa kama makapi, nao wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu." Kwa hiyo lisome Hilo, uone kama hiyo si kweli. Mnaona? Bali Yesu kamwe hakusema hivyo, Yeye alirejea kwenye Malaki 3, "Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia kwa ajili Yangu." Hiyo ni kweli kabisa.

231 Sasa, lakini kumbukeni, huyu mwingine alikuwa airejeshe imani ya watoto kwa baba zao, kuirejesha imani ya watoto kwenye Imani ya baba, Biblia asili.

232 Hivyo ndivyo Musa alivyofanya hasa. Hivyo ndivyo Yesu alivyofanya hasa. Hivyo ndivyo hasa kila mjumbe alivyofanya kote katika Biblia, kwenye wakati wa mwisho wa kipindi hicho cha wakati, waliurejesha ule ujumbe. Hao watu, kupitia mashirika na kadhalika, walivurugika kabisa na kila kitu, katika siku hizo.

233 Wamefanya jambo lilo hilo siku hizi! Kwa hiyo tunamtazamia mjumbe. (Mungu, mtume!) Mnafikiri tutampokea? La, bwana! Yeye atakuwa ni "mwendawazimu na mlokole," kweli kabisa, bali Mungu atamthibitisha. Mwaminio wa kweli, hao waliokusudiwa Uzima wa Milele, Yesu alisema, "Wote alionipa Baba watakuja kwangu, na hapana mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu. Na wote ambao Baba" (wakati uliopita) "amenipa Mimi, watakuja." Hiyo ni kweli, walikuwa . . .

234 Siamini katika mafundisho haya hapa ya Kibaptisti ya—ya usalama wa Milele. Ninaliamini kwa njia fulani, bali ninaamini wewe ni salama mradi tu uko katika Kanisa. Bali unatoka kwenye . . . kutoka chini ya Damu ya Yesu Kristo, wewe si salama. Niko salama na mvua mradi tu niko hapa ndani.

235 Na wakati umebatizwa katika Roho Mtakatifu na *kusema* unaye Roho Mtakatifu, kisha ulikane Neno la Mungu? *Kusema* uliamini na kumpokea Roho Mtakatifu, na kisha ukane kwamba Neno ni la kweli? Basi huyo anawezaje kuwa ni Roho Mtakatifu wakati Yeye Ndiye aliyeiandika Biblia? Ati Roho Mtakatifu alikane Neno Lake Mwenyewe, aseme, "Ni—nilikosea, wewe unasema kweli"? La, huyo si Mungu. La, bwana.

236 Upanga mkali! (Bwana, tutumie Ujumbe mkuu.) Huo ndio tunaoutazamia. Halafu, bila shaka, wakati anapokuja kuyatengeneza mawe hayo na kuyakata kwa ajili ya jengo, itakuwaje? Wengi wao hawatastahimili jaribio la Neno. Watapenda dhehebu lao kuliko wanavyolipenda Neno la Mungu, ingawa Neno hilo lithibitishwe na mtu huyo. Yeye atakuwa ni nabii atakayekuja katika Jina la Bwana, naye atakuwa ndiye atakayekuja juu ya nchi. Ninaamini hilo.

Loo, kila mtu anasema, "Itakuwa ni kundi la watu."

237 Ninataka mtu anionyeshe katika Biblia ambapo itakuwa ni kundi la watu; Mungu angelivunja Neno Lake Mwenyewe, Yeye hawezi kufanya hivyo. La, bwana. Yeye aliahidi hili. Itakuwa ni mtu mmoja. Halafu kutakuwako na wengine pamoja naye, hakika, maelfu, waaminio wote wa Kanisa watakuwa pamoja naye, kila mahali.

238 Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, hakutakuwako na wengi sana wao watakaookolewa, kwa sababu Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Mnajua hilo? "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," (wahesabu) "ndivyo itakavyokuwa."

239 "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Mnaona ninalomaanisha? Loo, ndugu, afadhali tufanye hesabu, huenda ikawa kweli imechelewa kuliko tunavyodhania. Huenda ikawa tutaamka siku moja na kuona ya kwamba tumekosa jambo fulani. Iweni waangalifu! Kesheni, ombeni, chunguzeni, tafuteni, msiliache Hilo lipite juu yenu. Pia, kumbukeni, Neno

la Mungu linapohubiriwa, Mungu anawajibika kwa Neno hilo na atalithibitisha.

240 Mnajua alichosema hapo, kile kilichotukia katika siku za Lutu? Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Ni nini kilitukia huko kabla tu ya moto kushuka? Itakuwaje tena kabla tu ya moto kushuka, ni ujumbe wa namna gani Kanisa litapata? Sio Sodoma sasa, Kanisa teule. Ziwekeni tu tatu hizo: wapo Wasodoma; na kulikuwako na Lutu na kundi lake, lile kanisa la kawaida; kulikuwako na Ibrahimu, Wateule. Wote watatu walipata ujumbe, naam, kwa wajumbe mbalimbali. Tazama ni wa aina gani aliyeliendea Kanisa teule, yale Yeye aliyomfanyia Ibrahimu. Yesu alisema, “Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, hatuwezi kukana hayo, hayo ndiyo Yesu aliyosema hasa. Kwa hiyo, hakika itakuwa hivyo.

241 Sasa, wengi. . .Yesu alipokuja na kuleta lile jaribio na kusema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi,” wangeweza kulistahimili jaribio? La. Na mtu yeyote anajua, maungamo yote ya mawe ambayo hayawezi kustahimili jaribio la Neno yanatupwa katika lundo. Limevunjika, maji yanavuja, halitastahimili jaribio. Loo, jamani, ndipo linatupwa kwenye lundo la takataka! Mungu daima amehesabu tabia badala ya idadi.

242 Ninafunga. Samahani nimewaweka muda huu wote, sikukusudia kufanya hili. Hebu mimi kwa da—dakika moja tu, mbili, nitoe tamshi hili la mwisho, ndipo nitaondoka katika dakika moja. Natumaini ni—ni—nimesema jambo la kuwasaidia ninyi, mnaona, kuwafanya mchunguze. Mnaona?

243 Mungu daima amehesabu tabia, sio wafuasi. Na siku hizi tunafanya kinyume. Tunahesabu idadi, nguo nzuri, wenye matoleo mazuri, badala ya tabia. A-ha.

244 Elieza alijitahidi sana, mpaka akaipata tabia. Hiyo ni kweli. Atampata nani? Naye alimtumaini Mungu. Tabia ya nini? Tabia kwa ajili ya Isaka, bibi-arusi, ambaye Kanisa ni mfano wake. Mnajua hilo. Huo ulikuwa ni uzao wa kawaida wa Ibrahimu; huu ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Vema, kama Elieza, yule mjumbe aliyekuwa akimtafuta bibi-arusi na kujaribu kupata tabia, kama mtu huyo amekuja, mjumbe wa siku za mwisho, akijaribu kumtafuta Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo, yeye hatatafuta ufuasi wa kimadhehebu. Yeye atatafuta tabia iliyo tayari.

245 Angalia! Tabia nzuri kwanza, kisha kumfanya tayari apate kukutana na Isaka. Akiisha kuipata hiyo tabia, basi anamfanya kusimama muda mrefu kutosha kuusikiliza ujumbe kutoka kwa Isaka.

246 Huyo ni mjumbe wa siku za mwisho, Nuru ya jioni, ni kwanza apate Kanisa hilo (watauaminia huo Ujumbe wapi?), utafute. Hivi mnaweza kusoma yale ninayozungumzia? Kutafuta mahali Kanisa hilo lilipo ambalo hata litakuruhusu kuingia, ambalo halitafunga mlango usoni pako. Halafu ukiisha kufanya hivyo, basi umeipata tabia. Sasa laiti lingesimama kimya muda mrefu kutosha kuliambia jinsi ambavyo Bibi-arusi hana budi kuvalishwa! Hana budi kuvalishwa nguo. Simama kimya! Kama angeweza kupata . . .

247 Mwangalie maskini Rebeka akisikiliza kila neno, maskini moyo wake ulikuwa ukidundadunda. Yeye . . . A—alikuwa akimwambia. Sasa, umejitahidi sana, "Nitaenda wapi?" mpaka niipate hiyo tabia. Halafu nikiisha kuipata hiyo tabia, ndipo nimfanye asimame muda mrefu kutosha nipate kumwandaa kukutana na yeye. Loo, jamani, ni jambo zuri jinsi gani! (Laiti tungalikuwa na muda mwingi kidogo kwenye saa ile ya ukutani.) Kumfanya tayari; kusimama kimya kuusikiliza ujumbe wake. Elieza hakuwa akinena habari zake mwenyewe, bali alikuwa akinena juu ya yeye aliyemtuma. Naye alikuwa na zawadi za kuthibitisha kwamba alitumwa kutoka kwake. Amina! Alitaka kumvika kwa vitu hivi. Mnajua jinsi alivyomwandaa.

248 Laiti ningaliweza tu kumfanya anawe uso wake! Mnaona? Mwajua, ni—nilijisikia tu kuzuiwa juu ya hilo, kwa hiyo afadhali nikimye. Kwa vyovyote vile, nimesema ya kutosha, mnajua yale ninayozungumzia. Vema, sikilizeni, simameni tu kimya.

249 Angalieni, mjumbe wa wakati wa mwisho, kazi yake itakuwa ni kuwafanya watakatifu tayari, Bibi-arusi tayari kwa ajili ya Bwana-arusi. Huo utakuwa ndio Ujumbe wake. Sasa mnataka kujifunza ABC zenu kusudi mweze kujifunza aljebra baadaye? Wakati mihuri hii mingine iliyo upande wa nyuma itakapofunguliwa itafunuliwa tu kwao. Hiyo ni kweli. Jifunzeni ABC kwanza. *ABC* ni nini? "Daima Mwamini Kristo," [Kiingereza: Always Believe Christ—Mfa.] (sio kanuni yako ya imani), Kristo. Mnaona? Amini yale Yeye asemayo, sio yale mtu mwingine asemayo.

250 Kama ni kinyume, kama mtu fulani akiwaambia, "Ni sawa kwenu kukata nywele zenu, wanawake," mnajua anasema uongo. Biblia inasema ni vibaya. Kama akisema, "Unaweza kuwa shemasi na bado uwe na wake wanne ama watano," yeye anasema uongo. Hilo ni kinyume na Neno. Mnaona? Mambo haya mengine yote tunayonena habari zake, yaleteni kwenye Neno muone kama Neno ni la kweli.

251 Lirejesheni kanisa kwenye Neno. Sasa, huyu mjumbe wa Malaki 4 atafanya nini? Kuirudisha Imani asili, Imani ya ufufuo. Kwamba, walimwona Yesu akiisha kufufuka katika wafu, wakamwona akitenda kazi miongoni mwao.

252 Walikuwa ni watu wa maneno machache. Walitoka wakaenda wakalihubiri Neno. Loo, walihubiri muda mrefu, Paulo alihubiri usiku kucha wakati mmoja. Mnaona? Mtu mmoja akaanguka kutoka jengoni, akafa. Yeye akaulaza mwili wake juu yake, akamfufua tena, mnaona. Mnaona? Mnaona, akaendelea kuhubiri.

253 Sasa, angalieni walikuwa ni watu tofauti na hawa Ph., L.L., Q.U.S.T., na chochote unachotaka kuwaita, siku hizi. Ati nini? Inamtenganisha mjumbe na. . . Ujumbe, hasa, kwa mjumbe, utawatenganisha waaminio na wasioamini. Baadhi yao watajiweka sawa na Hilo, na wengine hawatafanya hivyo. Baadhi ya Lutheri. . . Baadhi ya Katoliki walijiweka sawa na Luther, wengine hawakujiweka sawa. Baadhi ya Walutheri walijiweka sawa na Methodisti, wengine hawakujiweka. Wengine wanajiweka sawa na Pentekoste, na wengine hawatajiweka. Baadhi yao watajiweka sawa na Nuru ya jioni, wengine hawatajiweka.

254 Utajuaje kama ni Nuru ya jioni ama siyo? Lijaribu na Neno (sio tu Neno *moja*, Neno *lote* likiwekwa pamoja), uone kama ni kweli ama si kweli. Loo, liko ndani ya kitu gani? Basi kama Ujumbe huu ukitoa thibitisho la Mungu akifanya yale aliyosema Yeye angefanya, nalo limelingana na Neno, basi Neno linathibitishwa kama nyakati zingine na jinsi manabii wengine walivyofanya.

255 Angalia wakati Ujumbe. . . wakati. . . Angalia wakati Ujumbe umekataliwa na watu, naye mjumbe anaonekana kushindwa kabisa, hawezi kupata mlango mwingine, hawezi kupata mahali.

256 Kama vile Bwana wetu alivyokuwa. Kumbukeni, wakati Yeye alipokuwa. . . Loo, wakati alipokuwa akiwaponya wagonjwa, Nabii kijana, "Loo, jamani! Yeye ni Jamaa mashuhuri!" "Aloo, Rabi, u hali gani?" Lakini siku moja Yeye aliketi chini akaanza kuwaambia Ukweli. Akapata kibali cha kanisa, wale watu. Maelfu wakamfuata. Alikuwa na wahudumu sabini waliomzunguka, mbali na wale kumi na wawili. Lakini siku moja alipokuwa amegeuza mkate katika. . . ama kugeuza. . . kuzidisha mikate, kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, maana Mungu pekee ndiye aliyeishusha mikate kutoka Mbinguni. Naam. Mnaona? Alizidisha mikate. Na mara baada ya hayo. . . Alikuwa ametembea juu ya maji, akafanya miujiza, na kufanya mambo aliyokuwa amefanya, kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa.

257 Halafu basi, Yeye alipofanya hivyo, aliketi chini na kuanza kuwaambia watu kweli tupu. Hao watu wakaondoka. Nao wale sabini wakasema, "Ai! Ni nani anayeweza kulisikia Hili? Hilo ni neno gumu. Unayararua yale tuliyodhani kweli yalikuwa ni

kitu kingine. Sasa, Wewe ni nani kutwambia mambo haya?" Nao wakaondoka.

258 Ndipo Yesu akaligeukia kundi Lake dogo, kama katika siku za Nuhu, kama katika siku za Sodoma, kasema, "Mnataka kwenda, pia?"

259 Ndipo Petro akasema yale maneno makuu, "Bwana, twende wapi?" (Mungu, tusaidie.)

260 Angalieni wakati Ujumbe umekataliwa naye mjumbe anaonekana ameshindwa, hapo ndipo Mungu anapojitokeza jukwaani, Ujumbe wake umekwisha.

261 Nuhu, (nikifunga sasa), Nuhu alihubiri kwenye mlango wa safina yake kwa muda wa miaka mia moja na ishirini, mpaka, wakati hatimaye walipomcheka kwa dhihaka, Nuhu aliingia safinani akiwazia ya kwamba . . . ingekuwa tu ni sawa. Mungu akaufunga mlango. Nao watu wakakaa hapo karibu waone litakalotukia. Siku saba aliketi hapo akiwaza na kuwazua, ndipo kwenye siku ya saba mvua ikaja. A-ha.

262 Musa, yeye alikuwa katika nini? Kwenye jukumu lake kabisa, akiwaongoza watu. Bahari ya Shamu ikamzuia. Alikuwa kwenye mwisho wa safari yake. Ilikuwa ni wakati huo ndipo Mungu alipokuja na upepo wa Mashariki akaigawanya bahari, mwishoni mwa safari yake.

263 Ilikuwa Danieli, akisimama kwenye ujumbe wake, "Sitajitia najisi kwa ulimwengu huu wa mfalme." Akisimama mkweli kwa Mungu, alikuwa papo hapo kwenye mwisho wa safari yake, ilionekana kana kwamba mwisho wa wakati wake ulikuwa umewadia, wakamtupa kwenye tundu la simba. Mungu akaja jukwaani.

264 Halafu asubuhi moja, huko mbali sana katika Babeli . . . Amina! Ninaweza kuangalia juu Mbinguni, ninaweza kuona Ki—Kiti cha Enzi, Malaika wamesimama karibu. Naangalia hapa chini Babeli, ninaweza kuona ta—tanuru linalowaka moto. Ninaweza kuwaona watoto watatu wamesimama pale, wakisema, "Mungu wetu anaweza kutukomboa." Mnaona? "Lakini hatuinamii sanamu yako, kwa sababu ni kinyume na Neno." Mnaona? "Tumesimama hapa."

265 "Vema," kasema mfalme, "pandeni kwenye vipandio, mnaenda kuteketezwa kwa moto." Mtu mkubwa mnene, mwishoni mwa mkuki huu, hawa hapa wanapanda vipandio, hatua kwa hatua, inakuwa joto zaidi na zaidi.

266 Ninaweza kumwona Malaika amesimama pale, mmoja, upande mmoja wa kile Kiti cha Enzi, akaunyakua upanga na kuuchomoa, kasema, "Baba, angalia kule chini, yale yanayoendelea! Acha nishuke chini, mimi ni Gabrieli, nitayabadilisha yale mandhari."

267 "Rudisha upanga wako kwenye ala, Gabrieli. Nimeyaona."

268 Huyu hapa mwingine anakuja, kasema, "Baba, mimi ni Pakanga, mimi ni mwangamizaji kwa maji. Katika wakati uliotangulia gharika, mwanadamu alitenda dhambi na kuwatesa watu Wako, na mimi—mimi nikaupindua ulimwengu wote ukawa dunia ya maji. Nitaifagilia mbali Babeli kutoka kwenye ramani asubuhi ya leo. Niache niende."

269 "Ninajua ungeweza, Pakanga, wewe ni Malaika mwaminifu. Unaona? Lakini, siwezi kukuruhusu uende, hii ni kazi Yangu. Ninaenda, Mwenyewe."

"Hapa, unawaona?"

270 "Nimewaangalia usiku kucha. Nimeusikia mkutano wao wa maombi. Nimeona msimamo wao kwa ajili ya Neno Langu. Nitakuwa huko kwa wakati mzuri." Loo, jamani! Ninaweza kumwona akisimama na mavazi Yake ya kifalme yakianguka kumzunguka, namna hiyo, na kusema, "Njoni hapa, Upepo wa Mashariki, Kaskazini, Kusini, Magharibi. Simameni pale chini ya ile radi pale, nitawapanda kama gari la farasi asubuhi ya leo. Ninashuka kwenda Babeli, ninaenda kubadilisha mandhari." Loo, ndugu, Yeye alikuwa pale pale kwenye wakati!

271 Macho yake yako kwenye shorewanda nami najua Yeye ananiangalia. Angali anaangalia usiku wa leo, akiniangalia, Yeye anakuangalia. Ameangalia kama tutasimama ama hatutasimama, maamuzi tutakayofanya, kama tutasimama wa kweli kwa Neno ama tutaliacha. Wakati umeenda kuliko mnavyodhania.

272 Yakobo, akiwa njiani kwenda nyumbani, amevuviwa kurudi nyumbani, ndugu yake alikuwa akimlaki. Loo, lakini usiku mmoja alipigana mwereka na Mungu. Aliogopa kukutana na ndugu yake, lakini kesho yake asubuhi hakuwa na woga, mtawala anayechechemaa. "Simhitaji Esau wala jeshi lake, si mojawapo," Mungu aliingia jukwaani. Mnaona, Yeye anafanya katika njia ya kipekee.

273 Yesu, alikataliwa, baada ya kuwa Mwana wa Mungu aliyethibitishwa, kasema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi." Yeye alikuwa ndiye Nuru ya siku hiyo (Yeye angali ni Nuru!), akajitokeza jukwaani. Nao watu, mradi tu Yeye angeweza . . . mkate na samaki na mikate, walimfuata. Bali alipoanza kuwaambia Ukweli wa Neno, hilo liliwatenganisha, walikuwa na mapokeo yao wenyewe waliyoyashikilia. Ilikuwa ni kinyume, hata hivyo mnajua Yeye alikuwa pamoja na Maandiko kabisa. Lakini hayo macho yaliyopofushwa ya ulimwengu yasingeweza kuliona Hilo; wala hawajui, wala hawajajua katika wakati wowote, ninamaanisha, kwa jumla. Ni jambo gani lililotukia? Ilionekana kana kwamba Yeye alishindwa.

274 Angalieni, tangu wakati uo huo, umaarufu Wake ulimwacha. Lini? Hapo alipoanza kuwaambia Neno. Wakati angeweza kwenda na kuwa—na kuwa na ibada za uponyaji na miamsho,

kila mtu alimtaka, “Ee Rabi, njoo huku!” na, “Rabi, njoo hapa!” Lakini wakati Fundisho Lake lilipoanza; “Loo, Mafundisho Yako yanawasumbua watu wetu.” Loo, salala! “Loo, siwezi kukualika Wewe kanisani mwangu tena, Rabi, kwa sababu, mbona, Wewe unawafanya watu wetu wachanganyikiwe, Mafundisho Yako ni kinyume sana na yale tunayoamini.” Haijabadilika. Mnaona? Haijabadilika. Naam. “Hatuwezi kukualika Wewe, Rabi!” Hata hivyo Yeye amethibitishwa, akahakikishwa na Maandiko kwamba alikuwa ni Nani Yeye, hata hivyo wasingeamini Hilo.

275 Hatimaye akaendelea mpaka dakika ya mwisho, wakati Shetani alipowazia “Nimempata,” akamsulubisha msalabani. Akaendelea kushuka, kushuka, kushuka, mpaka hatimaye wakawazia kwamba walikuwa wamempata, wakamlaza kaburini. Lakini hapo ndipo Mungu alipojitokeza jukwaani. Huyo akafufuka kutoka kaburini! Kwa nini?

276 Jambo lile lile, Paulo, yeye alisema, “Wote...Dema ameniacha. Watu wote wameniacha kwa sababu ya Neno.” Siamini Dema alienda kwenye vilabu vya usiku na kadhalika. Lakini Dema alitaka kwenda, Dema alikuwa ni mtu tajiri. Naye alitaka kuambatana na kundi maarufu, na kwa hiyo akaenda kule ambako hao wengine wote walienda. Ndipo basi Paulo akasema, “Watu wote wameniacha.” Kwa nini? Huduma yake, alikuwa anakuja kwenye jiwe lake la kifuniko, akielekea mwisho wake.

277 Shauku yake ilikuwa ni kuwa mfia imani kwa kuwa yeye alimwua Stefano, alishuhudia kifo chake na kukiidhinisha. Alitaka kufa. Wakati ninii...Agabo, yule nabii anayejulikana, aliposimama karibu naye na kumwambia asiende Yerusalemu, yeye alisema, “Ninajua nisiende. Lakini si kwamba tu ninapenda kwenda, kwenda katika pingu na nimefungwa, hata Yerusalemu, bali niko tayari kwenda na kufa kwa ajili ya Bwana Yesu.” Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikuwa akiitia muhuri huduma yake.

278 Ee Kanisa la Mungu aliye hai, tungeweza kuzungumza usiku kucha. Tutautiaje muhuri Ujumbe wetu? Tutafanyaje hilo? Mungu, tusaidie kulichukua Neno hili, tusimame imara. Acha nife kwa Neno; niishi kwa Neno, nife kwa Neno. Itawanyeni Nuru, kwa kuwa wakati wa jioni kutakuwako Nuru. Tuko kwenye saa hiyo, enyi marafiki. Hebu tuliamini, tunapoviinamisha vichwa vyetu.

279 Kwanza, naomba msamaha kwa kuwaweka muda huu wote, kwenye saa mbili kamili, saa moja na dakika arobaini na tano, nafikiri, hasa. Natumaini ya kwamba hakuna kitu kimedhuru. Haitupasi kukoseana. Hilo, ikiwa hilo liko katika ninii yetu—ikiwa hilo liko moyoni mwetu na nafsini, basi tumekosea, sisi wenyewe, kama sisi wahudumu tukisema tu mambo hayo,

ndugu zangu hapa, hawa watu waliojazwa na Roho Mtakatifu. Mnaona?

280 Nilipookoka na kumwambia mchungaji wangu wa Kibaptisti ya kwamba nilikuwa nimempokea Roho Mtakatifu, na mambo haya yote, haya . . . na Malaika wa Bwana akaniambia la kufanya, yeye alisema, "Hapana shaka umekuwa na jinamizi, Billy."

Nikasema, "Daktari Davis, nilimwona Malaika."

281 Akasema, "Loo, upuuzi!" Kasema, "Hilo ni—hilo ni la ibilisi." Mnaona? Loo, jamani, jinsi hilo lilivyonikera! Akasema, "Ati utawahubiria wafalme na watawala?"

Nikasema, "Hilo ndilo Yeye alisema."

Akasema, "Ukiwa na elimu ya darasa la saba?"

Nikasema, "Hilo ndilo Yeye alisema."

282 Akasema, "Unafikiri ni nani atakayesikiliza? Ati utoke uende ukahubiri uponyaji wa Kiungu katika siku kama hizi, na utafiti wote mzuri wa tiba na kadhalika?"

Nikasema, "Siwezi kujiepusha ni Magoliathi wangapi wanaosimama kule."

Akasema, "Unafikiri ni nani atakayekusikiliza?"

283 Nikasema, "Kama Mungu ananituma, kutakuwako na mtu wa kunisikiliza."

284 Sikujua juu yenu nyinyi watu wakati huo. Na wakati nilipowajia, ilikuwa ni kama kutia glavu mkononi, nilishikamana kabisa nanyi. Nawapenda. Nawapenda. Nawapenda ndugu zangu wachungaji. Mnafikiri Mpresbiteri, Mmethodisti, ama Mlutheri, wangelifungua kanisa lao kama huyu ndugu alivyofungua usiku wa leo, kwetu kuketi hapa na kuhubiri ujumbe wa aina hii? La, bwana, hata kidogo. Hawa ni mashujaa wanaoamini Kweli. Sasa jinyosheni kwa Neno pamoja nao, mnaona, kaeni mbali na mambo ya ulimwengu.

285 Kina dada, acheni nywele zenu zikue. Vaeni nguo zenu, vizuri na nadhifu. Aibu kwako. Ondoa hiyo rangi usoni mwako. Unaona? Mna maandiko zaidi ya kujipodoa kuliko mliyo nayo ya kukata nywele zenu. Hiyo ni kweli. Msifanye hivyo. Msifanye hivyo. Biblia ilisema ni jambo la aibu kwa mwanamke kufanya hivyo. Nywele ni utukufu wake. Sasa mnasema, "Hilo ni jambo dogo." Hilo ni sawa, hebu tuyaondoe mambo madogo njiani ndipo tuweze kuzungumza juu ya mambo makubwa. Hebu na tuanze vizuri.

286 Sasa, ndugu zangu. Loo, jamani! Hebu niseme jambo moja kwa wanaume. Bwana, ndugu yangu, kama utamwacha mke wako afanye jambo kama hilo, ninakuonea aibu, nawe unadai kuwa ni mtu aliyejazwa na Roho. Aibu kwako, kumwacha mke wako aende mtaani.

287 Na nguo yako ni ya kizinifu sana na kila kitu namna hiyo, na hivi unajua ya kwamba Biblia ilisema, Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amezini naye"?

288 Unasema, "Sasa ngoja kidogo, ndugu yangu, mimi sina hatia." Ninaamini huna pia, dada yangu, wewe huna hatia katika tendo la kawaida. Lakini ukijianika naye mwenye dhambi akuangalie, na wewe ulijianika mwenyewe namna hiyo, ni nani mwenye hatia? Ni wewe, kwa kujianika. Ndipo kwenye siku ya Hukumu, hapo huyo mwenye dhambi atakapotoa jibu kwa kufanya uzinzi, yeye aliufanya na nani moyoni mwake? Wewe! Kwa nini? Kwa sababu ulijianika mwenyewe. Sasa, hiyo ni Kweli tu.

289 Hivi wewe, hivi, dada, tafadhali, katika Jina la Yesu, hebu nikuombe kama ndugu yako, hivi hutajirekebisha?

290 Ndugu, aibu kwako kwa kuendesha nyumba yako namna hiyo, jilainishe. Ni—nina matumaini bora kwako kama mwanamume. Unaona?

291 Wachungaji wanaowaruhusu watu hao kuingia, wanawachukua mashemasi na kadhalika na majukumu kama hayo, wakiwa na wake wawili ama watatu walio hai, na kadhalika, hivi huna aibu, ewe mhudumu? Hivi huyaonei mambo hayo aibu? Na kuwaingiza hao wafuasi humo ndani wakati wanaishi katika uzinzi, na kuvuta sigara, na kufanya yote, wala hata huyataji kutoka jukwaani. Aibu kwako! Na—na—nawaombea, ndugu.

292 Mungu awabariki. Asanteni kwa subira yenu ya kuvumiliana nami. Sasa, sijui . . .

293 Nuru ya jioni imekuja. Nuru ya jioni iko hapa, rudini kwenye Neno.

294 Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mioyo yenu imeinamishwa, jiulizeni swali hili, "Hivi niko sawa na Neno hili? Niko sawa?"

295 Ombi langu ni kwamba, kutoka jukwaani, "Ee Mungu, katilia mbali kila kitu kutoka kwangu kisichofanana na Wewe. Ee Mungu, kiondoe kwangu." Tuko chini hapa kwenye mwisho wa safari yetu.

296 Vema, mwaweza kuwa waaminifu hivyo kuinua mikono yenu na kusema, "Mungu, katilia mbali kutoka kwangu kila kitu ambacho si kama Wewe. Nifanye, Bwana, nifinyange mimi na unifanye"? Bwana awabariki.

297 Kama kuna mtu yeyote ambaye si sawa, naye ni mwenye dhambi na ameingia humu usiku wa leo, wala kamwe hajamkubali Kristo kama Mwokozi, ama aliyerudi nyuma ama kitu fulani, naye anataka kurudi, unaalikwa kuja kusimama hapa madhabahuni. Endapo unaamini ya kwamba Mungu angeyasikia maombi yangu kwa ajili ya wagonjwa, ninaamini

angenisikia. Na mimi na wewe pamoja tunapoiweka imani yetu juu ya ile Dhabihu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na kuomba dua, ninaamini Mungu atasikia. Umealikwa kuja na kusimama kwa ajili ya maombi.

298 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, tunakupa Wewe kusanyiko hili, maneno haya yaliyovunjikavunjika ambayo yamekuwa marefu, Bwana. Hata wengi wamechoka na kudhoofika na kwenda nyumbani, na labda wengine walijisikia vibaya kidogo, na, Bwana, si—siwezi kabisa kujua ni nani aliye kwenye kusanyiko wakati wote. Na, hata hivyo, Baba, ni Neno Lako na Wewe unaujua moyo wangu. Kwa hiyo . . . na mimi . . . Ole wangu nisipofanya hivyo. Na mimi—mimi sina budi kulifanya, Bwana. Kwa hiyo ninaomba sasa ya kwamba watu walio na ufahamu wa Neno watafahamu vizuri kabisa, nami nina hakika wale ambao Wewe umewaitia Uzima watafahamu, kwamba si kitu chochote ulimwenguni ila ni moyo uliojaa upendo wa Mungu na Kanisa Lake ambapo ninayatetea mambo haya.

299 Baba, karibu kila mkono humu ndani uliinuliwa kwa ajili ya tohara, kukatilia yote ya ziada ambayo si ya hapo. Mungu, tusaidie sote. Ninasimama moja kwa moja pamoja nao, Bwana. Mimi ni mmoja wao, ninakutazamia kule kuja kwa ile siku nzuri ya ule Utawala wa Miaka Elfu wakati dhambi na aibu zitaangamizwa milele. Basi, Baba, wakati tukiwa humu ulimwenguni tunajua ya kwamba tunashikamana na mambo haya, tu wanaokosea, tu watu watendao dhambi, tungali tunatembea, na hata hivyo hatupendi kufanya hivyo. Kama Biblia ilivyosema, "Usizimie moyo unapokemewa." Lakini ninaomba, Baba, ya kwamba kukemewa kwa Neno kutanikata vikali tu kama kunavyowakata hao wengine. Pia ninaomba, Baba, kwamba watalifahamu hivyo.

300 Ninaomba ya kwamba utawabariki sasa. Na jalia hili, kama tulivyoomba hapo awali, Bwana, tukijua na kuangalia yale tuliyoomba, kwa sababu hatutaki kuomba vibaya, hatutaki kuomba jambo fulani ambalo ni kujitungia tu maneno, kwa sababu tunazungumza na Wewe.

301 Ninakuomba Wewe umbariki maskini ndugu yetu hapa aliyeufungua mlango wake kwa ajili yangu kuingia usiku wa leo. Ninaomba ya kwamba Wewe utalibariki kanisa lake na ujalie kila mmoja wa washiriki wake, Bwana, aninii tu . . . Jalia hili liwe mnara wa taa, mahali ambapo karama za Mungu zinabubujika na kila kitu kikiendelea vizuri.

302 Mbariki kila mhudumu anayeketi hapa, makanisa yao. Pia jalia kuwe na mtikiso mkubwa sana, ama uvumi kwenye mforsadi, wa Roho wa Mungu akipitia Phoenix, na kuyaleta makanisa kwenye ushirika na kwenye—na kwenye uamsho mkuu, hata wahudumu hawataweza kuhubiri, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu; lakini wakati watakatifu wanapokusanyika

pamoja mapema alasiri, kule kulia na kuomba na kushuhudia na jumbe, kumwagwa tu halisi kwa Roho, wakati mji mzima utavutiwa kuja, ukasikilize. Tujalie sasa.

303 Waponye wagonjwa miongoni mwetu, Bwana. Wape ukombozi wa Kiungu, Baba, kupitia Jina la Yesu Kristo.

304 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama kuna yeyote hapa anayetamani kusimama papa hapa karibu na madhabahu sasa, na wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, nasi tutavumisha tu wimbo mdogo, wimbo m—m—mzuri wa kale, wa Injili. Nasi tunataka kuuvumisha huo. Basi tutakapofanya hivyo, kukiwako na mtu yeyote anayetaka tukuombee, u—upate ujuzi wenye kilindi, kumpokea Roho Mtakatifu, ama umeokoka na hujatakaswa bado, ama chochote kile, tutafurahi kufanya hivyo wakati tukiuvumisha wimbo huu mdogo, *Nampenda*. Na ikiwa unampenda, hebu tuliheshimu Neno Lake sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

305 Wanapokuja, ninataka kila mmoja achukue mahali pao hapa sasa. Vema, dada.

. . . mpenda, nampenda
Kwani Yeye . . .

Njoni sasa, kuyazunguka madhabahu, ninyi mnaotaka kuja sasa.

. . . mimi
Na kununua wokovu wangu
. . . Kalvari

306 Kwa nini baadhi yenu dada mlio na nywele fupi msije huku na kumtolea Mungu ahadi? Mnataka niwasomee kutoka katika Biblia? Vema. Hivi hamtakuja, mseme, "Bwana, ninataka kuwa sawa katika mambo yote, nami ninataka kuanza vizuri. Nami ninataka kuingia kwenye barabara nzuri na kukaa mle. Nitatoa ahadi Kwako usiku wa leo, Bwana. Itakua tangu sasa na kuendelea"?

307 Biblia ilisema ni aibu kwa mwanamume kuwa na nywele ndefu, kuonekana kama mwanamke. Mungu alifanya maagano mawili, moja na Adamu na moja na Hawa. Aliwavalisha tofauti. Wao ni tofauti, kwa jumla. Daima wamekuwa tofauti. Kunayo maagano mawili kote katika Biblia. Ningetaka kuhubiri juu ya maagano hayo mawili usiku mmoja, wakati mmoja, kuwaonyesha tofauti yake ni nini. Loo, jamani, ni zuri sana. Hata yako kwenye kesi zenu za ndoa na talaka, kama tu mlijua ukweli juu ya hilo, ingetatua suala hilo lote. Hiyo ni kweli. Vema, tena sasa, wakati tukiwa na hakika sasa. Njoni, sivyo?

Nampenda, . . .

Mnamhitaji Roho Mtakatifu? Njoni huku, simameni huku.

Kwani alinipenda kwanza
Na . . .

Mnataka kutembea kwa karibu pamoja na Yeye? Njoni, wekeni nadhiri, simama karibu na Yeye na uitimize. Haitafaa kitu kuweka nadhiri isipokuwa uitimize.

Juu . . .

Unaweza kuja uweke nadhiri yako. Mungu hana budi kuijaza. Wewe shikilia tu nadhiri yako.

308 Sasa nitawauliza ndugu zangu wahudumu kama mtatembea mshuke hapa sasa, msimame moja kwa moja mkiwazunguka watu hawa wa thamani tunapoomba papa hapa, zungumzeni na kila mmoja, waulizeni haja zao sasa wakati tukiwa hapa.

309 Kila mtu akiwa na kicho tu uwezavyo. Sasa, Mungu atawaheshimu, iweni tu na kicho kabisa mpaka mstari huu wa maombi utakapofanyizwa. Mnaweza kuja kuzunguka moja kwa moja sasa, hapa ndani, karibu, juu na nyuma ya watu hawa wanaosimama hapa kwa ajili ya maombi.

Mtini Kalvari.

310 Sasa tena, wakati kukiwapo na wahudumu wamekusanyika pande zote mbili.

Nampenda, na . . .

Ninapenda kuona hilo, wahudumu wa madhehebu mbalimbali, wote katika umoja sasa; hapo ni chini ya Damu.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari. (Jamani!)

311 Sasa tembeeni huku, ndugu, moja kwa moja kwenye mtu wako unayesimama karibu naye, weka mkono wako juu yao na uwaulize wanachohitaji kutoka kwa Mungu. Huu ni wakati wa ajabu sana? Mwajua, ninapoona jambo hili, angalieni hapa, wahudumu wa makanisa mbalimbali, wamesimama pamoja. Dada waliokuwa kwenye vitanda vya wagonjwa wameamka, wakatoka, wakaenda. Bwana asifiwe. Tunashukuru sana kwa jambo hilo, tukisimama katika Jina la Bwana.

312 Sasa, hebu kusanyiko sasa, kila mmoja inamisha kichwa chako. Kila mmoja wenu sasa, moyoni mwako, zungumza tu na Mungu kama vile ungezungumza nami; kama vile ungekuja huku na kusema, “Ndugu Branham, mimi—mimi . . . ” Kama umetenda kosa, sema, “Samahani, Ndugu Branham. Ni—nilifanya hili, utanisamehe kwa ajili yake? Nitakutolea ahadi, Ndugu Branham, kamwe sitafanya hivyo dhidi yako tena.” Sasa badilisha tu kutoka jina langu, kutoka kwangu, kwenda kwa Bwana wako Yesu Kristo.

313 Na kama unahitaji uponyaji, kama vile ungekuja useme, "Ndugu Branham, ni—nimefilisika, sikula chakula chochote cha jioni usiku wa leo, na, naam, ninajua kama ulikuwa na dola ungenipa." Sasa, unaona, haikubidi kumwambia Mungu, "Kama unazo nguvu za uponyaji." Anazo, unaona. Ingekulazimu kuniambia, *"Kama* unazo." Bali Kwake haikubidi kusema, *"Kama* Wewe unazo." Yeye anazo! Unaona? Kwa hiyo unasema, kama vile, "Ndugu Branham, waweza kunipa dola moja? Na—na—nataka chakula." Mbona, hakika ningekupa, unajua hilo. Kama nilikuwa nayo ningekupa, wakati wowote. Ningekuwa na moyo mbaya sana kama sikukupatia. Nami, nikiwa mtu katili, mwenye dhambi, nami ningekuwa na moyo safi hivyo kwa mtu kama wewe, Mungu angekuwaje?

314 "Kama ninyi mkiwa waovu mnajua kuwapa vipawa vizuri, ni zaidi sana vipi Baba yenu wa Mbinguni atawapa Roho Mtakatifu, hao waombao." "Kama ukiomba samaki, angekupa nyoka? Ukiomba mkate, Yeye angekupa jiwe?" La hasha!

315 Mbona, kama ungemwomba tu kwa njia hiyo, kwa imani, ukiamini ya kwamba, utapata kutoka Kwake upesi mara milioni moja kuliko vile ungepata chochote kutoka kwangu. Nawe unajua ningekusaidia, ningefanya lolote niwezalo. Yeyote wa ndugu hawa angekupa, tungetafuta kila peni kutoka mfukoni mwetu kukusaidia. Tungefanya chochote tuwezacho. Lakini hiki ni kitu ambacho huna budi kuamini kwa imani.

316 Sasa, amini kwamba utapokea tunapoomba, nanyi muombe, na kusanyiko liombe, nami ninaamini Mungu atashuka na kuyajibu maombi yetu. Na dakika ile ile utakayohisi kwamba umepata, kwamba Mungu atayajibu maombi yako, basi ulifanya agano, "Bwana, nilikosea, sitafanya hivyo tena. Nitainua mkono wangu, ninakuahidi ya kwamba sitakosea," Mungu ataamini usemalo. Nawe liamini tu jinsi hiyo nalo litakwisha. Basi inueni tu mikono yenu na kumshukuru Yeye, "Bwana, nimefanya nadhiri yangu sasa. Nami ninajua ya kwamba ni Yako, na Wewe uliahidi kuyajibu, wala huwezi kushindwa."

317 Baba wa Mbinguni, sisi, watumishi Wako, tunasimama juu ya kundi hili ambalo limejitokeza likihitaji baraka Zako na usikivu Wako kwenye wakati huu. Baba, hao ni tunu za Ujumbe, wakati wa Nuru ya jioni. Wengi wao, Bwana, wanakiri. Wengine wao wana haja sana. Naomba, Mungu, kwamba katika Jina la Yesu kwamba Wewe hutamfukuza mmoja wao, kwa kuwa Wewe utalitimiza Neno Lako. Ninakukumbusha Neno Lako, Bwana, kama vile Petro alivyofanya pamoja na wanafunzi hapo walipoomba katika Matendo 4, walisema, "Bwana, likumbuke Neno! Kwa nini makafiri wamefanya ghasia, na watu wakatafakari ubatili?"

318 Sasa, Baba, tunalileta Neno Lako. Wewe ulisema, "Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele. Yeye anijiaye Mimi

sitamtupa nje kamwe. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

319 Loo, dua zetu na zijulikane kwa Mungu, na Yeye atatujibu. Yeye kwa wingi. . . "Yeye atakayekiri dhambi zake atapata msamaha. Yeye azifichaye dhambi zake hatafanikiwa." Nasi tunakiri makosa yetu. Ninakiri makosa ya hawa watu. Ninakiri makosa yangu mwenyewe. Naomba rehema. Ninaomba uponyaji. Ninaomba neema. Naomba ya kwamba utammwaga Roho Mtakatifu, Bwana, sasa hivi juu ya watu hawa wanaongojea, kwamba maisha yao yatabadilishwa katika bloku ya Mungu ya kufinyanga, na yatachongwa katika sura ya Mwana wa Mungu, ili kwamba Roho aliyemhuisha, kwamba ataingia ndani ya mwili wao na kuwafanya wana na binti za Mungu. Tujalie, Bwana.

320 Tunaamini kwamba Wewe upo. Tunaamini ya kwamba utaliheshimu Neno Lako. Tunaamini utaziheshimu jitihada za Neno. Sasa tuma baraka hizi juu ya watu hawa wakati wakiungojea Uwepo Wako kuwatembelea hapa madhabahuni. Katika Jina la Yesu.

321 Sasa, kama unaamini, na unaamini ya kwamba ulipokea, inua mkono wako kwa Mungu. Kama unayakubali kama maombi ya imani na nadhiri yako wakati sasa ukimgeukia Mungu, inueni mikono yenu.

322 Basi kusanyiko na lisimame. Kila mtu, asimame, anayetaka kumtolea Mungu ahadi, sasa useme, "Ninaliamini. Ninalikubali Hilo. Ninaamini Hilo."

323 Sasa inueni mikono yenu na kumpa Yeye sifa na yote yatakwisha. Utukufu kwa Mungu! Asante, Bwana Yesu, kwa ajili ya wema Wako na rehema Zako, na kwa yote uliyotufanyia sisi, Bwana. Tunakupa Wewe sifa kupitia Yesu Kristo.

*MJUMBE WA JIONI* SWA63-0116
(The Evening Messenger)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumatano jioni, tarehe 16 Januari, 1963, katika Pentecostal Church Of God huko Mesa, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org